# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumapili Aprili 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581660

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

JUMAPILI

LIKE & FOLLOW US




**Mwinyi** ahimiza ushirikiano na Saudi Arabia

UKURASA 2



**Waziri** akuta harufu wodini huku watumishi wakidai stahiki

UKURASA 3

**Biteko**: Serikali kushirikiana na sekta binafsi sekta ya elimu

UKURASA 5



## Silva bado hakieleweki Man City

UKURASA 22



# Siri upigaji serikalini hii

• CAG mstaafu aonyesha tatizo lilipo, trilioni 2.78/- zahofiwa kuliwa kifisadi mwaka mmoja... *ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SAMIA ATOA MSAMAHA KWA WAFUNGWA 1,082

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha kwa wafungwa 1,082 ambapo 29 kati yao wameachiwa huru juzi na wengine 20 waliokuwa wakitumikia adhabu ya kifo wakibadilishiwa adhabu...

UKURASA WA 7

### VIJANA HAWA WANATOA WAPI UJASIRI HUU?

ZAMANI tulipokuwa tukijiunga na kidato cha kwanza baada ya kufaulu darasa la saba na si kuchaguliwa kama inavyosemekana leo, tulitangulia kwenda shuleni kabla wenyeji hawajawasili...



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Mgeni wake, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia, Dk. Hassan Sheikh Mohamud wakiangalia burudani ya ngoma za utamaduni, wakati alipowasili katika viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## ACT yasema haitakubali kuhujumiwa uchaguzi

UKURASA 2

# Tanzania yaahidi kuisaidia Somalia kurejesha amani

UK. 2

**MICHEZO** **BENCHIKHA ADAIWA KUOMBA KUONDOKA SIMBA** UK.24 **MAONI,** UK.6

## Mwinyi aahidi ushirikiano na Saudi Arabia

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameihakikishia Serikali ya Saudi Arabia ushirikiano mzuri uliopo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwenye miradi mbalimbali ya Maendeleo.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Mawasiliano, Ikulu Zanzibar ilisema Rais Mwinyi alisema hayo alipozungumza na Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Ahmad Okeish, na ujumbe wake, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano ulioko baina ya nchi mbili hizo.

Dk. Mwinyi alisema SMZ ni mnufaika mkubwa wa mifuko ya Saudia na Kuwait katika miradi yake ya maendeleo kupitia ushirikiano mzuri ulioko baina ya mataifa hayo.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliishukuru na kuipongeza serikali ya Saudi Arabia kwa ushirikiano wake na Tanzania hususan kuipatia zawadi mbalimbali inazozituma kwa watu wa Zanzibar zikiwamo tende wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Katika salamu zake kwa Tanzania, Balozi Okeish alipongeza mafanikio makubwa yaliyofikiwa na taifa hili kwa kutimiza miaka 60 ya Muungano wake baina ya Tanganyika na Zanzibar, sambamba na kuuombea mafanikio zaidi.

Pia Balozi Okeish alisifu ushirikiano wa diplomasia ulioko baina ya nchi hizo mbili ikiwamo Zanzibar pamoja na tamaduni.



Mwendesha mkokoteni akiwa kausheheni madumu matupu ya plastiki katika barabara ya Kawawa, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kitendo kinachomfanya kushindwa kuona nyuma jambo ambalo ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania yaahidi kuisaidia Somalia kurejesha amani

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, wamefanya mazungumzo na kukubaliana kuendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali, huku Tanzania ikiahidi kuunga mkono jitihada za kuirejeshea amani nchi hiyo.

Marais hao wamekubaliana na mawaziri wa kisekta na wataalam wakiratibiwa na mawaziri wa mambo ya nje, wakutane wazungumze halafu waibue maeneo ya kushirikiana. Wakizungumza baada ya mazungumzo yaliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam jana, maraisi hao pia walikubalinana kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kuwa na mfumo rasmi wa kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo.

Rais Mohamud ambaye yuko nchini kwa ziara ya kikazi, akiambatana na ujumbe wake, juzi alikuwa miongoni mwa marais walioshiriki sherehe za miaka 60 ya Muungano wa Tanzania.

“Tumemshukuru sana kwa kukubali mwaliko wetu wa kufanya ziara ya kiserikali hapa kwetu, ni ziara ya kwanza ya kiserikali hapa nchini tangu aingie madarakani na ni ya kwanza ya kiongozi wa kitaifa wa Somalia tangu ijiunge na Jumuiya ya Afrika Mashariki, hii ni ziara ya kihistoria.

“Tumemshukuru pia, kwa heshima aliyotupa ya kushiriki nasi katika sherehe za miaka 60 ya Muungano,” alisema.

Rais Samia alisema kadri wanavyokuwa wamoja katika nchi ndivyo wanavyokaribia kujenga mtangamano wa Afrika, hivyo hawana budi kuhakikisha wanadumisha umoja kama walivyodhamiria waasisi wao na wa Umoja wa Afrika.

Alisema katika mazungumzo rasmi ya kiserikali waliyofanya wamegusia maeneo mengi ya kimkakati na muhimu, ukiwamo uhusiano wa kiplomasia licha ya wananchi wa Somalia na Tanzania kuwa na uhusiano na mwingiliano kwa miaka mingi.

“Ziara hii imetupa fursa kujadili uimarishaji wa uhusiano baina ya nchi zetu. Tumeona kuna umuhimu wa kuwa na mfumo rasmi wa kuimarisha uhusiano huo. Ni dhamira yetu kuimarisha mikutano ya mashauriano baina ya nchi zetu mbili, kupitia wadau wetu wa kisekta ndiyo tutaibua maeneo na miradi yenye manufaa kwetu sote,” alisema.

Rais Samia alisema Tanzania inapongeza jitihada za Rais huyo na serikali yake katika kuendeleza vipaumbele vyake vya kitaifa na usimamizi wa ajenda ya usimamizi wa taifa lao, kupitia mashauriano ya kisiasa.

Pia alisema sema wanaipongeza Somalia kwa jitihada zake za kuendelea kurejesha amani na usalama katika nchi yao, kama Ujumbe la Baraza la Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika na pia, majukwaa mengine Afrika, hivyo Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada za kurejesha amani .

Alisema serikali ya Somalia imekuwa ikichukua hatua kubwa na za kupongezwa katika masuala ya uchumi na kijamii na wamekubaliana, kuimarisha uhusiano ikiwamo masuala ya kijamii hususani eneo la afya na elimu.

Naye, Rais Mohamud alisema ziara hiyo ni heshima kubwa kwao kwani ni sehemu ya kupanua mipaka ya uhusiano baina ya nchi hizo na hivyo, amemshukuru Rais Samia kwa ukaribisho huo.

Alisema Tanzania imekuwa washirika wa karibu ambao wanataka kuendelea kufanya nao kazi na kushirikiana nao miaka ijayo.

“Tunataka kuendeleza hili kusudi katika msingi ya kuheshimiana na kushirikiana katika maeneo mbalimbali yanayotunufaisha sote. Nimefurahia majadiliano ya leo tumeangalia maeneo ya kimkakati ili kutia nguvu uhusiano wetu.

“Yale yote ambayo serikali yetu imesema tutayafanya ili kudumisha ushirikiano huu na kujenga mifumo mizuri kusaidiana kiuchumi ,” alisisitiza.

Alisema serikali ya Somalia ina mifumo mbalimbali ya kutengeneza uchumi na wameweza kushusha deni la taifa na kutokana na historia nzuri, Somalia imefanikiwa kuondoa zuio la silaha lililowapo kwa muda mrefu.

# ACT Wazalendo yasema haiko tayari kuhujumiwa uchaguzi ujao Zanzibar

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHAMA cha ACT Wazalendo, kimesema wakati taifa linapoelekea kwenye uchaguzi mkuu ujao, hakiko tayari kushuhudia hujuma za uchaguzi, kisha kusubiri wale waliowahujumu waje mbele yao wameinamisha shingo.

Aidha, kimetoa wito kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, asijiingize kwenye orodha ya marais, ambao katika zama zao walishiriki kumwaga damu ya Wazanzibar.

Akizungumza jana katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa mkutano mkuu wa kidemokrasia wa ACT Wazalendo (MMK) na miaka 10 ya mapambano na matumaini, Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bara, ambaye pia ni Waziri Mkuu Kivuli, Isihaka Mchinjita, alisema ACT Wazalendo inajiandaa kwenda kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, na wanakwenda kuiongoza Serikali ya Zanzibar.

“Ni vyema sana Rais (Dk. Hussein) Mwinyi asijiingize kwenye orodha ya marais ambao katika zama zao walishiriki kumwaga damu ya Wazanzibar. Huu ndio wito wetu ACT Wazalendo tunautoa kwa Rais Mwinyi. “Namweleza wazi kwamba, hatuko tayari kushuhudia hujuma za uchaguzi kisha kusubiri wale waliotuhujumu waje mbele yetu wameinamisha shingo kana kwamba hakuna walichofanya,” alisema

Kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi, Mchinjita alisema hawana tatizo la maoni yaliyotolewa na Kikosi Kazi cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa yapo na yamewekwa hadharani na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Samia Suluhu Hassan), na leo unaweza kwenda kuyaona.

Hata hivyo, alisema shida yao ni maoni ya Kikosi Kazi cha Zanzibar, akidai yameshikiliwa na hayajafanyiwa kazi.

“Nataka niwaambie wana mabadiliko wote, na wapigania demokrasia Zanzibar. ACT Wazalendo, itashirikiana nao kuhakikisha kwamba mabadiliko yanafanyika,” alisema.

Katika ufunguzi wa kongamano hilo, Kiongozi mpya wa Chama Cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, akieleza hali ya nchi kiuchumi kwa miaka 10, akiyataja mambo matano yanayotakiwa kudhibitiwa ili kuliepusha taifa kufarakanika na kuendeleza utegemezi, hata baada ya miaka mingi ya uhuru wa kisiasa.

“Mambo ambayo tulieleza yanayoitafuna nchi yetu na kufuja rasilimali za umma ni kama vile ufisadi mkubwa unaotegeneza mabilionea na kuwaacha maskini mamilioni, utoroshwaji wa fedha unaofanywa na kampuni za kimataifa (illicit financial outflow) tafiti zinaonesha Tanzania inapoteza fedha wastani wa shilingi trilioni 2.1 kila mwaka.

“Sehemu kubwa inafanywa na Kampuni za Kigeni na na sehemunyingine nibakshishi wanayopewa viongozi namaafisa wa serikali wanaofanikisha utoroshaji huu. Vilevile, uingiaji wa mikataba ya madini, gesi, mafuta na uwekezaji mwingine bila kuzingatia uhitaji wakuboresha mazingira ya nchi kufaidikana utajiri wa rasilimali zetu.

# Samia atoa msamaha kwa wafungwa 1,082

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha kwa wafungwa 1,082 ambapo 29 kati yao wameachiwa huru juzi na wengine 20 waliokuwa wakitumikia adhabu ya kifo wakibadilishiwa adhabu na kuwa kifungo cha maisha.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alisema wafungwa hao wamepata msamaha huo ikiwa ni maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika taarifa hiyo iliyotiwa saini na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Daniel Sillo, kwa niaba ya Waziri, wafungwa 27 waliohukumiwa kifungo cha maisha wamebadilishiwa adhabu na kuwa kifungo cha miaka 30.

Ilisema pia kuwa wafungwa 1,006 wamepunguziwa adhabu zao na watabaki gerezani na kuendelea kutumikia sehemu ya kifungo kilichobaki.

"Ni matarajio yetu serikali kuwa wafungwa walioachiliwa huru leo Aprili 26, watarejea tena katika jamii kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa taifa na kwamba watajiepusha na makosa ili wasirejee tena gerezani," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema wafungwa wote wenye sifa stahiki wapunguziwe robo ya adhabu zao wanaozitumikia hivi sasa baada ya kutoa punguzo la kawaida la moja ya tatu linalotolewa chini ya kifungu cha 49 (1) cha Sheria ya Magereza Sura ya 58.

Pia ilisema wafungwa hao sharti wawe wamehukumiwa robo ya adhabu zao gerezani na wawe wameingia gerezani kabla ya Desemba 28, 2023, isipokuwa wafungwa walioorodheshwa katika sharti la 2(i-xi).

Kadhaliaka, ilisema wagonjwa wenye magonjwa ya kudumu au sugu ambao wapo kwenye hatua ya mwisho, ugonjwa na hatua hiyo vidhibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya.

"Wafungwa wa kike walioingia na ujauzito gerezani au wenye watoto wanaonyonyesha au wasionyonya. Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili wasio na uwezo wa kufanya kazi.

"Ulemavu huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu/ Mganga wa Wilaya. Wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 10 au zaidi," ilisema taarifa.

Kadhalika ilifafanua kuwa, baadhi ya makosa ambayo hayahusiani na msamaha huo ni wafungwa wanaotumikia vifungo vya nje na wale waliowahi kukiuka masharti ya vifungo vya nje ya Sheria ya Bodi ya Parole Sura ya 400 (R.E 2002), Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 (R.E 2002 na kanuni ya kifungo cha nje.

Pia ilisema wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifugo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji fedha, rushwa na usafirishaji au kujihusisha kwa namna yoyote ile na dawa za kulevya ikiwamo bangi.

"Wanaotumikia kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya wizi au ubadhirifu wa fedha za serikali. Makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kutendeka kwa makosa hayo," ilisema.

Kadhalika ilisema msamaha huo hauwahusu wenye makosa ya waliojaribu kuua, kujaribu kujiua au kuua watoto wachanga, ugaidi, uharamia na makosa ya kimtandao.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Tundu Lissu akiwa juu ya gari wakati akiongoza maandamano ya chama hicho, mjini Singida jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Waziri akuta harufu wodini watumishi wakidai stahiki

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKATI watumishi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tabora ya Kitete iliyoko mkoani hapa watumishi wake wakidai hawajalipwa stahiki zao zaidi ya miezi minne, hali ya usafi wa wodi ya wazazi hospitalini hapo si nzuri na kuchangia kuwapo kwa harufu.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amekutana na changamoto hiyo baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika hospitali hiyo inayopokea zaidi ya Sh. milioni 267 kila mwezi.

Akiwa katika kikao baina yake jana na watumishi hao, alibaini changamoto hizo, huku akisema amefika hapo baada ya kuambiwa hospitali inanuka na hilo amejionea alipoingia katika moja ya wodi ya wazazi na kukuta hali ya usafi siyo nzuri.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watumishi hao walieleza kukabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo hayajashughulikiwa na uongozi kwa muda mrefu, licha ya hospitali hiyo kuingiza mapato kila mwezi, hivyo kuwavunja moyo katika utendaji.

Walizitaja baadhi ya kero hizo kuwa ni kutolipwa stahiki zao kwa muda mrefu ikiwamo fedha za likizo, matibabu, kutopandishwa vyeo na marupurupu mengine ya kiutendaji.

Kadhalika walilalamikia hali ya mazingira ya hospitalini hapo kutoridhisha hususan katika wodi ya wazazi na maeneo mengine, licha ya kuwapo kampuni iliyopewa kandarasi ya kufanya usafi ikidaiwa kutokuwa na uwezo wa kazi na uongozi kuendelea kuitumia.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Mark Waziri, alithibitisha kuwapo kwa kero hizo pamoja na hospitali kuendelea na utekelezaji wa jukumu la kutoa huduma za afya kwa weledi kwa jamii.

Hata hivyo, alisema changamoto tajwa zinasababishwa na kupungua kwa fedha za matumizi mengineyo (OC) walizokuwa wanaletewa.

Mhasibu wa hospitali hiyo, Samwel Mgula, alithibitisha stahiki nyingi za watumishi kutolipwa tangu mwezi Januari hadi sasa kutokana na ukosefu wa fedha, kwa kuwa fedha wanazoletewa kila mwezi hazitoshelezi.

Kutokana na hilo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Mollel alisema serikali inatoa Sh. milioni 267 kila mwezi hospitalini hapo lakini amebaini fedha hizo ziko mifukoni mwa baadhi ya viongozi wa hospitali na kueleza kuwa, hali hiyo haikubaliki, huku akiahidi kuchukua hatua dhidi yao.

"Kwa fedha hizo zote mnazopokea kila mwezi mnashindwaje kuwalipa watumishi stahiki zao na mbaya zaidi wana madai ya muda mrefu, katika hili menejimenti mmeshindwa kazi, tutafanya uamuzi," alisema.

Dk. Mollel aliongeza kuwa kabla hajafika hospitalini hapo aliambiwa kuwa hospitali inanuka na amelithibitisha hilo ni kweli, kwani ameingia katika moja ya wodi ya wazazi na kukuta hali ya usafi sio nzuri.

Alisema hali ya usafi hospitalini hapo hairidhishi na kuonyesha uongozi umeshindwa kazi na hivyo kuahidi kuwachukulia hatua stahiki watumishi wote wasiowajibika ipasavyo ili kuboresha utoaji huduma.

Naibu Waziri huyo alielekeza Timu ya Afya ya Mkoa (RHMT) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kusimamia utendaji wa hospitali hiyo wakati wizara ikilifanyia kazi suala hilo na kuahidi kurudi ndani ya wiki mbili ili kutoa uamuzi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa huo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Deusdedit Katwale, aliahidi kuendelea kusimamia weledi katika suala zima la utoaji huduma za afya katika hospitali hiyo, huku akiahidi kuwa wiki mbili alizowapa watazitumia kufanya marekebisho ya kiutendaji.

MAKALA

# Siri upigaji serikalini hii

Na Mwandishi Wetu



MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, (pichani) amesema kukosekana uadilifu ndicho kiini cha kuendelea kuripotiwa vitendo vya rushwa na ufujaji wa fedha za umma.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati Taasisi ya WAJIBU ambayo yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wake, ilipowasilisha uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23.

Uchambuzi wa taasisi hiyo unaonesha kuwa fedha za serikali ambazo ziko hatarini kupotea kutokana na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni Sh. bilioni 1,770.84 kwa mwaka 2019/20, Sh. bilioni 4,590.73 mwaka 2020/21, Sh. bilioni 3,084.55 mwaka 2021/22 na Sh. bilioni 2,778.01 mwaka 2022/23.

Amesema dosari hiyo kiutendaji inatokana na watumishi wa umma kukosa uadilifu, hivyo kutumia fedha za umma kwa manufaa yao binafsi.

Alitoa mfano, utata ulioripotiwa na CAG katika ripoti yake ukaguzi wa mwaka 2022/23 ambamo anasema Wizara ya Maliasili na Utalii iliingilia katika mazingira yenye utata zabuni iliyotolewa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Mamlaka hiyo ilitangaza zabuni ya ujenzi wa jengo la makao makuu yake ambayo mshindi wake alitangazwa Machi 9, 2022 baada ya mchakato wote wa zabuni kukamilishwa kisheria, zabuni ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 9.8.

Hata hivyo, CAG anaripoti kuwa Aprili 21, 2022 zabuni ilisitishwa kwa maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii, iliyoagiza zabuni itangazwe upya, lakini mshindi akawa yuleyule alishinda zabuni ya kwanza, lakini kukawa na ongezeko la Sh. milioni 686.6 kutoka Sh. bilioni 9.8 za awali hadi bilioni 10.4. Pia kukawa na gharama nyingine ya mchakato wa zabuni Sh. milioni 16.08.

Akifafanua hoja yake, Utouh alisema: "Tatizo si sheria, tatizo ni sisi na ukosefu wa uadilifu. Hilo ndilo tatizo letu kubwa. Na huu mfano wa NCAA, ninawashukuru TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kusema kwamba mnalichunguza.

"Iko wazi kwamba ile ni mtu aliona zabuni imepita, 'itapitaje mimi sijapata changu? Akaagiza zabuni isitishwe. 'Rudieni', halafu akaweka hapo cha kwake. Liko wazi hili, ni suala la uadilifu".

Utouh alisema wakati mwingine yatakuwa yanafanyika marekebisho ya sheria, lakini hayatakuwa na maana kama watumishi wa umma na jamii haitakuwa na uadilifu.

"Hata huu mfumo mpya wa ununuzi wa umma (NeST), ni mfumo mzuri, lakini tumekuwa na matatizo nchini, watu kukataa kutumia mifumo.

"Sasa swali ni hili, kwa NeST hii, mtakuwa na mbinu gani ya kulazimisha watu ambao wanakataa kutumia mifumo kwa sababu zao binafsi za kujinufaisha?", Utouh alihoji, akielekeza hoja kwa watendaji wakuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) waliokuwamo ukumbini wakati wa wasilisho la uchambuzi huo.

Alisema katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (halmashauri), kuna sheria ya kutumia mashine za POSS, lakini CAG kila anapokagua anakuta fedha zimekusanywa na hazijapelekwa benki.

"Kwahiyo, hoja si mfumo, bali hoja ni uadilifu wetu sisi. Na ninafikiri hili tupigie kelele sasa nani atamfunga paka kengele? Serikali ni watu; mimi, wewe na yule, Mama Samia na kila mtu, ndiyo serikali! Na kinachoporwa na kinachopigwa ni mali ya nani? Ni mali yako wewe na mimi.

"Tufanyaje? Ni vikao kama hivi tuelimishane, kupeana taarifa ili sisi wananchi tupige kelele. Tukipiga kelele, hiyo serikali ambayo imetulia, itashtuka, itaamka na kuchukua hatua.

"Kwa hiyo, mimi niseme kwamba kubwa ninaloliona mimi, yote haya ya rushwa na 'madudu' mengine serikali ukweli ni tabia zetu, ni ubinafsi wetu, ile tamaa ya kujilimbizia mali, ambayo imekubuhu kwa watumishi wengi wa serikali na hata watumishi wa sekta binafsi.

"Rushwa iko pande mbili. Si tu kwamba rushwa iko kwa watumishi wa serikali, mara nyingi nao wanapigwa na sekta binafsi.

"Rushwa iko kote, serikalini na sekta binafsi, ingawa zinazopigwa nyingi zaidi ni za serikali kwa sababu ni rahisi kuzipiga zile. Ndiko zinapigwa nyingi zaidi," alisema, ukirejewa uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2021/22, uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, umebainishwa miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Katika uchambuzi wake, taasisi hiyo imebaini kwamba kiasi ambacho aidha hakikukusanywa au kimetumiwa na serikali pasi na kupata tija yoyote (nugatory expenditure) kimepungua kwa asilimia 33 kutoka Sh. bilioni 4,590.73 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Vilevile, uchambuzi umebaini kuwa mashirika ya umma yamekuwa na ongezeko la asilimia 43 ya jumla ya miamala ambayo ina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kutoka Sh. bilioni 1,408.36 mwaka wa fedha 2020/21, hadi Sh. bilioni 2,015.78 mwaka wa fedha 2021/22.

Hii ina maana kwamba jumla ya miamala yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika mashirika ya umma pekee ni Sh. bilioni 2,015.78 sawa na asilimia 65 ya jumla ya miamala yote yenye viashiria vya rushwa ubadhirifu na udanganyifu ya Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa ujumla, katika uchambuzi wake huo, Taasisi ya WAJIBU imebainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, ikisababisha hatari ya upotevu wa Sh. bilioni 1,770.84/- mwaka 2019/20, Sh. bilioni 4,590.73 mwaka 2020/21 na Sh. bilioni 3,084.55 mwaka 2021/22.

Hii ina maana kwamba, jumla ya Sh. trilioni 9.446 ziko hatarini kupotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika miaka mitatu ya fedha (2019/20-2021/22).

Kiasi hicho kama kingelielekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kingelitosha kujenga vyumba vya madarasa mpya 472,306 au matundu milioni 8.587 ya vyoo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote huku tundu moja la choo likijengwa kwa Sh. milioni 1.1.

Sh. trilioni 9.446 zilizo hatarini kupotea, kama zingeelekezwa kwenye sekta ya afya, zingetosha kujenga hospitali 1,246 za wilaya au vituo vya afya 8,056 au zahanati 31,419.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ujenzi wa zahanati unagharimu wastani wa Sh. 300,641,028 (vifaa vinagharimu Sh. 87,677,593.70); ujenzi wa kituo cha afya unagharimu wastani wa Sh. 1,172,583477 kikiwa na majengo 11 (vifaa vinagharimu Sh. 501,728550) huku ujenzi wa hospitali ya wilaya ukigharimu Sh. bilioni 5.781 (vifaa vinagharimu Sh. bilioni 3.4).

Kimsingi, kuwapo hatari ya upotevu wa fedha za umma iliyoibuliwa na CAG ilhali nchi inakabiliwa na uhaba wa miundombuni na samani shuleni, kunakwaza utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

Mpango huo umebainisha malengo muhimu katika sekta ya elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026, ambayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote, malipo yao na makazi kuwa karibu na maeneo ya kazi.

Hatari hiyo ya upotevu wa mabilioni ya shilingi ilhali nchi bado inakabiliwa na uhaba wa vituo vya kutolea huduma za afya, unakwaza utekelezaji wa Sera ya Afya (2007) na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2008 unaoelekeza serikali kuhakikisha kunakuwa na zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na hospitali kwa kila wilaya nchini.

| MWAKA | SH. BIL |
|---|---|
| 2019/20 | 1,770.84 |
| 2020/21 | 4,590.73 |
| 2021/22 | 3,084.55 |
| 2022/23 | 2,778.01 |

**Fedha ambazo ziko hatarini kupotea kutokana na viasharia vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu serikalini kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji - Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu ya Taasisi ya WAJIBU, Aprili 2024.**

# Biteko: Serikali itaendelea kushirikiana na shule binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi, hususan shule binafsi ili kuboresha sekta ya elimu nchini.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi Tanzania (TAPIE) jana jijini Dar es Salaam, Dk. Biteko alisema serikali haiwezi kuacha wadau wa elimu wakilalamika kwa kuwa uwapo wao unaisaidia serikali.

"Nataka niwahakikishie serikali imeendelea kukutana na TAPIE mara kwa mara na hapa namwelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, kuratibu mkutano wa pamoja kati ya TAPIE na Wizara za Ardhi, Fedha, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kujadiliana kwa pamoja na kupata suluhu ya changamoto zinazowakabili," alisema.

Dk. Biteko pia aliitaka TAPIE kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika barua na vyeti vya usajili wa asasi zao kwa kuwa kuna baadhi hukiuka masharti, hivyo kusababisha migongano isiyo ya lazima na mamlaka zilizokasimiwa kusimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya uendeshaji wa asasi za elimu.

Pia aliitaka kufuata sheria na kanuni za utoaji elimu, kuhimiza na kuimarisha maadili, nidhamu na malezi bora kwa watumishi na wanafunzi walio chini ya asasi zao.

Alisema suala la uadilifu katika shughuli za uendeshaji na usimamizi wa mitihani ya kitaifa lisisitizwe na kutiliwa mkazo ili kupata wataalam wenye sifa stahiki.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alizipongeza shule binafsi kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambao sasa unavutia baadhi ya wanafunzi kutoka nchi zingine kusoma nchini

"Tunapozungumza kuwa tunaenda na elimu ya miaka 10 tunaamini sekta binafsi ina msaada mkubwa katika hili kwa sasa. Tutaanza na ujenzi wa shule 100 za sekondari za ufundi na ni imani yangu kuwa tutashirikiana vizuri na sekta binafsi", alisisitiza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, alisema serikali imeweka mazingira wezeshi katika sekta binafsi na sasa kuna zaidi ya shule 500.

"Tunaipongeza sekta binafsi kwa kutoa ajira na Bunge tunatambua mchango wa TAPIE. Tutawaunga mkono katika kuboresha sekta hii ya elimu.

## Bodaboda wakumbushwa kutimiza wajibu kisheria

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema mabadiliko ya sheria yaliyofanyika Julai 2023 yanataka wafanyabiashara na wamiliki wa pikipiki maarufu kama bodaboda kulipia Sh. 65,000 kama kodi ya shughuli za usafirishaji wanazozifanya.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TRA Mkoa wa Kagera, Castro John, wakati akitoa taarifa ya robo mwaka katika ukusanyaji wa mapato kwa mkoa huo.

Alisema bodaboda wamekuwa wakifanya shughuli zao bila kutoa kodi kama wafanyabiashara wengine ambao wanafanyiwa makadirio ya uzalishaji shughuli zao kwa mwaka.

Alisema kodi hiyo inatakiwa kulipiwa kwa awamu nne, ambapo robo moja ya mwaka mfanyabiashara huyo atalipa Sh. 16,200.

"Tumekuwa tukizungumzia suala hili kupitia vikao, lakini mwitikio wa bodaboda kuja kufanyiwa makadirio ni kidogo, na tayari sheria imeshapitishwa na siyo lazima mtu alipe kwa pamoja, ataweza kulipia kidogo kidogo hadi anakamilisha malipo ya mwaka," alisema John. Alisema endapo malipo yakikamilika atapatiwa utambulisho wa chombo chake kwa kupewa stika ya mapato ilifanyiwa makadirio.

John alisema jambo lingine ambalo limekuwa tatizo katika kwa vyombo vya moto ni ubadilishaji umiliki pindi chombo kimeuzwa.

Alisema kufanya hivyo ni kumwepushia malalamiko mmiliki wa pili endapo chombo hicho kilikuwa kikifanya au kitafanya uhalifu.

"Hii inasaidia kwani kumekuwa na malalamiko kwa watu kuwa, pikipiki imekamatwa ikifanya uhalifu sehemu na umiliki unasoma yule mtu wa kwanza au mtu ameinunua pikipiki inakwenda kufanya uhalifu," alisema Castro.

John alisema kinachotakiwa ni kubadilisha vitu kama mkataba, unaoambatana na kadi na uhamisho wa umiliki.



Daktari wa GGML aliyebobea katika magonjwa yatokanayo na kazi, Cretus Karwan (kushoto), akichukua damu kwa mmoja wa vijana waliotembelea banda la GGML na kupatiwa huduma za awali za upimaji wa afya katika maonyesho ya OSHA yanayoendelea jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yaja na teknolojia za kisasa maonyesho ya OSHA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuelimisha wananchi na washiriki wa maonesho ya usalama na afya mahali pa kazi namna ya kuzingatia usalama wawapo katika shughuli zao, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imeleta vifaa mbalimbali vya kisasa ili kutoa fursa kwa washiriki hao kujifunza teknolojia za kisasa za uokoaji.

Hayo yamebainishwa na Meneja Usalama kutoka GGML, Isack Senya, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho hayo yanayofanyika kwenye viwanja vya General Tyre jijini Arusha na kuratibiwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

"Kama kawaida GGML kwa kutambua umuhimu wa afya na usalama kazini na ikiwa ni tunu yetu ya kwanza, GGML ina wawakilishi zaidi ya 45 kwenye maonesho haya wanaotoa elimu mbalimbali kuhusu masuala ya afya na usalama kazini," alisema Senya. Alisema katika maonyesho hayo wamekuja na vifaa mbalimbali ikiwamo rada maalumu ambayo ina uwezo wa kutambua ukuta ambao una udhaifu au unaoweza kuanguka pindi shughuli za uchimbaji mgodini zikiendelea. Senya Alisema rada hiyo hutoa ripoti mapema ili kuondoa watu kwenye maeneo husika iwapo ukuta au mwamba huo unataka kuanguka.

"Kifaa hiki kinaangalia eneo la uchimbaji na kinavyozunguka kinapiga picha za satellite. Picha hizi zinarejeshwa kwenye mfumo na kuona kama kuna mwenendo wowote wa ukuta unaoweza kuleta athari, inamtahadharisha mtaalamu na kuchukua hatua stahiki.

"Rada hii ilisaidia sana mwaka 2007 ambapo kulitokea maporomoko makubwa sana ya ukuta lakini kutokana na kifaa hiki, yalibainika mapema na kuchukua hatua stahiki ikiwamo kudhibitiwa," alisema.

Alisema pia timu ya GGML imekuja na mambo mengi zaidi na tofauti kulingana na kaulimbiu ya mwaka huu inayosema 'Mabadiliko ya Tabianchi na Athari za Usalama na Mazingira".

"Tumeona madhara mbalimbali yaliyotokana na mabadiliko ya tabia nchi hivyo tumeona ni muhimu sasa kuhakikisha elimu zetu tunazotoa zinajikita kwenye maeneo hayo," alisema na kuongeza pia katika banda hilo wanatoa huduma za awali za afya ikiwamo upimaji wa magonjwa ya kisukari na presha.

Mbali na rada pia alisema GGML wameleta boti ya uokoaji majini, vifaa vya uokoaji katika uchimbaji chini ya ardhi pamoja na kutoa elimu kuhusu majanga makubwa na vidhibiti majanga ambayo yanaweza kuepukwa.

Alisema katika maonesho hayo tayari wameshatoa mafunzo ya namna ya kujikinga na kukabiliana na majanga ya moto kwa mamalishe 50 wa mkoani Arusha pamoja na kuwagawia mitungi ya gesi ya kupikia.

Pia alisema wanatarajia kutoa mafunzo kwa madereva pikipiki kuwaelimisha namna ya kuzingatia usalama pindi wawapo katika shughuli zao.

Alisema kutokana na mifumo imara ya udhibiti majanga pamoja na kuzingatia masuala ya afya na usalama kazini kwa muda wa zaidi ya miaka 14 sasa ndani ya GGML hakuna kifo kilichotokea kutokaa na shughuli hizo za uchimbaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendeshe siasa kistaarabu kwa amani na ustawi wa taifa

**VUGUVUGU** la uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwakani, limeanza kushika kasi huku kukiwa na matamko mbalimbali ya viongozi wa vyama vya siasa.

Mbali na matamko hayo yenye viashiria vya kupanda kwa joto hilo, pia baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wamekuwa wakifanya ziara katika mikoa mbalimbali kwa lengo la kuvijenga vyama na kutafuta uungwaji mkono.

Katika ziara za viongozi wa vyama hivyo, Chama Cha Mapinduzi ambacho kwa sasa kinashika dola, wajumbe wa sekretarieti wamefanya ziara mara kadhaa kwa kile wanachokiita kukagua uhai wa chama na kusisitiza maendeleo. Hivi karibuni sekretarieti hiyo ilifanya ziara takriban mikoa yote na wajumbe wake kuweka misimamo ya chama katika masuala mbalimbali huku wakisisitiza kuwa nia ya chama hicho ni kuendelea kushika dola na kuendelea kuongoza nchi kutokana na imani waliyo nayo Watanzania kwao.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeendelea kuendesha siasa zake kwa kufanya maandamano katika kanda mbalimbali za kichama huku ajenda kubwa zikiwa kikokotoo cha mafao ambacho kimekuwa kikilalamikiwa na watumishi, kupanda kwa gharama za maisha na bidhaa ikiwamo sukari.

Licha ya ziara na matukio hayo ya kisiasa, kumekuwa na kauli na matamko kutoka kwa baadhi ya viongozi ambayo yamekuwa na viashiria vya kwenda kinyume cha misingi ya kidemokrasia na hali ya amani na utulivu nchini.

Mmoja wa viongozi wa CCM mkoani Kagera, kwa mfano alisema watawapoteza baadhi ya wapinzani ambao wamekuwa wakikosoa serikali na polisi wasiwatafute. Mwingine naye akasema Watanzania wasio wanachama wa CCM ni wasaliti na wamemwasi Mungu. Hata hivyo, Katibu Mkuu wa CCM, alisimama na kusema Tanzania ni ya Watanzania wote bila kujali itikadi zao

Viongozi wengine wa vyama vya upinzani ambavyo vinaendesha siasa kama ilivyo CCM, nao wamekuwa wakitoa kauli mbalimbali ambazo zina ukakasi kama vile kuwataja viongozi wanaosababisha kupanda kwa bei ya sukari na bidhaa kwa madai kwamba wanawalazimisha wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa hizo nje ya nchi kuongeza fedha kidogo kwa madai ni maagizo kutoka juu.

Chama cha ACT Wazalendo nacho kimekuwa kikitoa kauli mbalimbali ikiwamo jana kwamba katu hakitakubali kuhujumiwa katika uchaguzi mkuu mkuu utakaofanyika mwakani, hasa ule wa Zanzibar.

Matamko hayo, yanakinzana na dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhusu kuendesha siasa kistaarabu na kwamba kila chama na wafuasi wake kiko huru kufanya mikutano na hata maandamano ilimradi visivunje sheria. Rais pia amekuwa akisisitiza maelewano, maridhiano na ujenzi upya wa taifa kupitia kile alichokiita R4.

Juzi, mathalan, Tanzania ilikuwa inatimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliozaa taifa la Tanzania huku viongozi wakuu wakihimiza Watanzania kuendelea kuulinda Muungano kwa ustawi wa taifa. Ustawi wa Muungano huo umetokana na kuwapo kwa amani, utulivu, umoja na mshikamano ambavyo ni nguzo katika kudumu kwake.

Ni dhahiri kwamba hakuna anayezuwia kufanya siasa katika utawala wa sasa lakini kinachosisitizwa ni kuendesha siasa za kistaarabu ambazo haziwaumizi wengine kwa njia ya matusi, hila na ghiliba. Serikali imeweka wazi suala hili, hivyo hakuna haja ya kusimama majukwaani na kutukana watu au kutoa kauli za vitisho. Huo si utamaduni wa Watanzania walioishi kwa amani na upendo bila kujali imani wala itikadi zao.

Ni vyema kila mtu anayefanya siasa, afanye huku akizingatia kwamba Tanzania ni ya watu wote walioko katika ardhi hii na hakuna mwenye hatimiliki ambaye anajiona ana uhuru wa kutoa kauli za matusi, vitisho na kashfa dhidi ya viongozi na Watanzania wengine. Ustaarabu ndiyo silaha yetu na tuudumishe kwa amani na umoja wa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kumhusisha Mungu na kadi za vyama vya siasa si sahihi

Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni, kuna mwanasiasa alikaririwa na mitandao ya kijamii akisema: "Wote ambao hawana kadi za CCM wamemsaliti Mungu. Haiwezekani umezaliwa Tanzania, kwa sababu nataka kuwaambia kuzaliwa Mchaga huchagui, kuzaliwa Mpare huchagui, kuzaliwa Tanzania huchagui, vyote hivyo umevikuta."

Mwanasiasa huyo anaendelea kusema; "Lakini wakati unavikuta unakuta Mungu naye kashaweka utaratibu wake, tokea tumepata uhuru mwaka 1961.

Yaani wote hapa tumezaliwa baada ya uhuru, tumekuta CCM iko madarakani. Na Biblia inasema mamlaka zote mtakazozikuta duniani zimewekwa na Mungu lazima mzitii.

"Sasa nakushangaa umezaliwa tena bahati nzuri umezaliwa Mndengereko, halafu umezaliwa Tanzania, Arusha halafu unakutana na mbunge ni mwana CCM, diwani CCM, mwenyekiti wa mtaa CCM, halafu wewe unajiita mpinzani. Si umemgeuka Mungu, wakikuita Yuda kuna ubaya?

Kwa sababu Mungu ndiye kaweka hizi mamlaka na kwa bahati nzuri mamlaka zinatoka CCM. Yeyote yule ambaye hana kadi ya CCM kwa Tanzania hii, kamsaliti Mungu bila kujua".

Nionavyo ni kwamba kumwingiza Mungu kwenye mzaha huo si sahihi, hivyo ni vyema wanasiasa wakawa wanafakari kwanza kabla ya kutoa kauli kama hizo wanapotafuta waanachama.

Mungu anahusikaje mtu kuwa na kadi ya chama fulani au kutokuwa na kadi? Uhusiano wa kadi ya chama na Mungu uko wapi? Mwanasiasa huyo hakuona mifano mingine hadi amhusishe Mungu?

Hizo kadi za vyama vya siasa zinatoka kwa Mungu hadi aseme kwamba mtu ambaye hana kadi ya chama hicho amemsaliti Mungu? Kwa hili huyo mwanasiasa ameteleza.

Mwanasiasa huyo ametoa kauli hiyo ikiwa ni wiki chache tangu mwingine wa mkoani Kagera atoe onyo lenye utata lililozua mjadala hadi Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, akaingilia kati.

Kiongozi huyo wa UVCCM, alikaririwa na vyombo vya habari akisema watu wanaotumia mitandao kumtukana Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake, muda wao kuendelea kufanya hivyo sasa umekwisha.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, kumekuwapo na tabia ya watu wanaotumia mitandao kumchafua Rais na viongozi wengi huku wengine wakiwa ni miongoni mwa viongozi wa CCM na kulitaka jeshi la polisi kutowatafuta watu hao watakapopotezwa.

Hata hivyo, kauli hiyo ya kupotezwa imepokewa kwa hisia tofauti na watu mbalimbali, akiwamo Dk. Nchimbi ambaye amepinga kwamba nchi hii si ya chama cha siasa ni yetu sote na kwamba akiibuka kijana wa CCM na kusema kuwa wapinzani wamefanya jambo fulani lazima tuwapoteze, atampinga.

Ninadhani umefika wakati wanasiasa kutafakari kwa kina na kuachana na kauli ambazo si sahihi, badala yake waimarisha umoja wa kitaifa badala ya kauli kama hizo zinazoleta ukakasi na taharuki ndani ya jamii.

Ingekuwa vyema kama watarudi kwenye mstari na utaratibu wa asili wa maadili, uungwana utu na heshima kwa wote, kwani kauli ya aina hiyo sidhani kama inakwenda sawa na utaratibu wa chama.

Hatua ya Katibu Mkuu wa CCM kukana kauli ya kiongozi wa Kagera, ni wazi inakwenda kinyume, hivyo ingekuwa nafasi nzuri kwa kiongozi na wengine wenye mihemko kama hiyo wakaachana nayo.

Ni vyema kama vijana hao kama wanaona kuna jambo la kujadili, basi walijadili kwa maslahi mapana ya nchi na kujenga hoja, kujadili mipango ya maendeleo, sio kauli zinazoleta utata.

Kauli tata za wanachama hao ni kama mwendelezo kauli ambazo zimewahi kutolewa na viongozi wengine wa ngazi hiyo katika baadhi ya mikoa na kuleta taharuki.

Sidhani kama kuna chama ambacho kinashabikia kauli zinazolenga kuwagawa Watanzania, hasa kwa kuzingatia kwamba wote ni wamoja, bila kujali tofauti za itikadi za vyama au hata wakiwa chama kimoja.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Pongezi miaka 60 ya Muungano, twende mbele zaidi hapa tulipo



Pascal Mayalla

JUZI, Watanzania waliadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania. Waasisi wa Muungano huo, Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa iliyokuwa Jamuhuri ya Tanganyika na Abeid Karume, walikubali kuachia madaraka ya kuongoza mataifa yao na kuanzisha taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muungano wetu ni adimu na adhimu kwa sababu hapa duniani, hakuna muungano mwingine wowote kama huu. Ni muungano wa nchi mbili kuungana na kuunda nchi moja ya Tanzania, yenye nchi mbili ndani yake, Tanzania na Zanzibar. Ni muungano wenye marais wawili, Rais wa JMT na Rais wa Zanzibar.

Si hivyo tu, ni muungano wenye Katiba mbili, katiba ya JMT na Katiba ya Zanzibar na wenye mabunge mawili - Bunge la JMT na Baraza la Wawakilishi, mahakama kuu mbili za ya Tanzania na Zanzibar.

**KUUNGANA TANU NA ASP**

Vyama vya TANU na Afro Shiraz (ASP) vilivyopigania ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar na hatimaye kufanikiwa, vilipoungana mwaka 1977, si Watanzania wengi walikuwa wamezaliwa!. Wengi wamezaliwa, wameikuta CCM, hivyo hawakuikuta TANU na ASP. Kwa mantiki hiyo, hawajui kwa nini TANU na ASP ziliungana na kuanzishwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), na viliungana ili iweje?

Mimi ni mtu wa miaka ya 1960, hivyo mwaka 1977, TANU na ASP zilipoungana, nilikuwa darasa la tatu, kijijini Itonjanda, nikikaa kwa bibi mzaa Baba, Bibi Wakawombwe (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi) baada ya Baba Mzee Mayalla (naye ametangulia mbele ya haki) kuhusika na yale mambo fulani ya Mwanza ya 1976. Sababu ya TANU na ASP kuungana ilikuwa kuelekea kwenye serikali moja. Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alisema huu muungano wa vyama vya TANU na ASP na kuzaliwa chama kipya, CCM, ni mwanzo wa safari ya kuondoka kwenye serikali mbili, kuelekea kwenye serikali moja. Je, ndoto hii ya Mwalimu Nyerere, kwa Tanzania kuwa nchi moja ya JMT yenye serikali moja na rais mmoja, itakuja kutimia?

Watanzania wanahitaji sana kuelimishwa kuhusu Muungano wetu adimu na adhimu. Tena ni Rais Samia Suluhu Hassan, ndiye kiongozi wa kwanza wa juu aliyetoa ruhusa watu waachwe huru kujadili Muungano. Baada ya Muungano, nchi zote mbili zilitoweka, hakuna nchi ya Tanganyika wala Zanzibar bali nchi ya Tanzania, nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili..

**ELIMU YA URAIA**

Duniani kuna miungano ya aina juu mbili. Kwanza ni ule ujulikanao kama 'Union'. Katika muungano huoo, nchi mbili au zaidi zinaungana kuunda nchi moja. Zile nchi zote zinakufa na inazaliwa nchi moja mpya.

Pili, ni muungano wa shirikisho. Katika aina hii ya muungano, nchi mbili au zaidi zinaungana na kuunda nchi moja lakini nchi zote zinakuwa na serikali ya muungano, maarufu kama 'Federal Government' lakini kila nchi inakuwa na utawala wake wa ndani.

Muungano wetu ni wa kipekee sana ndiyo maana unaitwa muungano adimu na adhimu. Sababu kubwa ni kwamba ni muungano pekee duniani ambao upande mmoja ni muungano kwa nchi mbili kuungana kuunda nchi moja na upande wa pili ni muungano wa shirikisho wenye serikali mbili, Ni muungano wenye marais wawili, mabunge mawili na mahakama mbili.

Muungano wetu kimataifa ni muungano wa 'union'. Tanzania kimataifa ni nchi moja ya JMT, yenye serikali moja ya JMT, chini ya rais mmoja wa JMT ambaye ni mkuu wa nchi, mkuu wa serikali na amiri jeshi mkuu. Lakini kitaifa, ni nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar, yenye katiba mbili - katiba ya JMT na katiba ya Zanzibar. Nchi yenye serikali mbili, serikali ya JMT na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), yenye marais wawili, rais wa JMT na rais wa Zanzibar

**MKANGANYIKO WA KATIBA**

Kama nilivyosema awali, kimataifa Tanzania ni nchi moja ya JMT na hakuna mkanganyiko wowote wa kimataifa kuhusu Tanzania. Lakini Kitaifa kuna mkanganyiko wa katiba kati ya katiba ya JMT na katiba ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa katiba ya JMT ya mwaka 1977, Tanzania ni nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar. Zanzibar si nchi bali ni sehemu ya JMT yenye utawala wake wa ndani.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, inaiita Zanzibar ni nchi. Ni moja ya nchi mbili zinazounda JMT. Kitendo cha katiba ya Zanzibar kuuita Zanzibar ni nchi kinawakanganya Watanzania kudhani kuwa nchi ya Tanganyika ndio pekee iliyokufa ila Zanzibar ipo na wala haikufa.

Naomba niwahakikishie Tanzania ni nchi moja ambayo niJMT, inayotajwa na katiba ya Zanzibar kuwa ni nchi ya Zanzibar, si kweli bali ni jina tu. Mabadiliko ya katiba ya Zanzibar kuwa ni nchi, kimuungano ni mabadiko batil, ila, kwa vile mabadiliko hayo ni kwa ajili ya Zanzibar tu na hayatambuliwi na katiba ya JMT, serikali ya JMT, imeamua kuyapuuza.

Lakini kutokana na hizi kelele, tutapuuza mpaka lini?. Si ni bora twende kwenye serikali moja haya yote yaishe?

Kwa vile Rais Samia anakwenda kutupatia katiba mpya, nashauri hili la mkanganyika wa katiba kati ya Katiba ya JMT na Katiba ya Zanzibar pia litarekebishwa. Kwa maoni yangu, dawa pekee ya uhakika na ya kudumu ambayo ni mwarobaini wa kuzimaliza kero zote za Muungano, ni kwenda kwenye serikali moja.

Nimalizie na hili swali, je, Tanzania sasa tumefika wakati wa kutimiza ndoto ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, ya uzalendo wa kweli wa JMT wa kwenda kwenye nchi moja, yenye serikali moja na rais mmoja?

**Hongera miaka 60 ya Muungano wetu adimu na adhimu.**

**Paskali +255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Vijana hawa wanatoa wapi ujasiri huu?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

ZAMANI tulipokuwa tukijiunga na kidato cha kwanza baada ya kufaulu darasa la saba na si kuchaguliwa kama inavyosemekana leo, tulitangulia kwenda shuleni kabla wenyeji hawajawasili.

Sisi tukiitwa 'njuka (new comers)' au 'wapya', tuliwahishwa ili kuzoea mazingira kabla wale wa kidato cha pili na kuendelea, hawajaripoti kutoka likizo ya mwaka ili kuanza mwaka mpya na kidato kipya.

Na walipofungua wenyeji kama wiki mbili baadaye, wale wa kidato cha pili walikuwa na shughuli nasi. Walitutesa kwa kile walichokuwa wakidai ni kututoa ugeni.

Sitaki kukumbushia hali iliyokuwa enzi hizo bali itoshe tu kusema tulipitia ya kupitia, nasi kufanya hivyo tulipokuwa kidato cha pili tukilipiza kisasi kwa wasio na hatia. Lakini ndio ulikuwa utaratibu ingawa si rasmi.

Niliripoti kidato cha kwanza katika sekondari iliyokuwa ya wavulana watupu ikiwa jirani na sekondari ya wasichana watupu lakini zote zikiwa na jina linalofanana huku 'Boys' na kule 'Girls'.

Hata hivyo, nilikuwa na rafiki aliyeniacha shule ya msingi huku yeye akichaguliwa kujiunga an sekondari hiyo, akiwa amenitangulia miaka. Nilifarijika kuwa na 'skulumeti', hivyo nikiamini nisingepitia mateso ya jamaa wa kidato cha pili.

Ingawa hiyo haikuzuia, sikula suluba kama walivyokula wenzangu kwa sababu jamaa yangu alikuwa mbabe fulani hivi, hivyo akanifanya kuwa 'lokaboi (lockerboy)' wake.

Lokaboi alikuwa kijana wa kidato cha kwanza aliyemhudumia wa kidato cha tatu, kumfuatia chakula bwaloni na kumwoshea vyombo na ilizoeleka yakawa maisha ya kawaida kwani lokaboi kuna nyakati alinufaika na huduma hiyo kwa chakula cha ziada.

Lakini kabla hatujaanza masomo rasmi, siku chache baada ya wenyeji kuwasili, siku moja jamaa yangu akanitaka nijianadae ili tutoke pamoja jioni, bila hata kuniambia safari ilikuwa ya wapi. Mimi nani nikatae!

Kwa kumwamini nilimwacha nje akiwa na wenzake, nikaingia bwenini kubadili nguo tayari kwa safari hiyo isiyojulikana mwelekeo wake. Nilikawia bwenini kiasi fulani na nilipotoka, sikumkuta na hata wenzake sikuwaona.

Kwa kuwa sikujua mweleko wa safari, nilirudi bwenini kubadili nguo na kuvaa za kawaida zisizo na uhusiano na safari, nikajifanyia mambo mengine jioni hiyo ikiwa ni pamoja na kujiandaa kumchukulia chakula.

Lakini kabla muda wa chakula haujawadia, zikasambaa taarifa shuleni kuwa kuna wanafunzi kutoka 'Boys' wamekwenda 'Girls' na kushambulia walimu waliokuwa wakiwazuia kuonana na wasichana!

Kweli, ghafla tukasikia kengele ikigongwa muda usio wake, tukajua lazima kuna dharura. sote tukatoka tulikokuwa na kwenda mstarini, tukakuta mwalimu wa zamu na wengine wakiwa wamehamanika.

Tulipotulizana msitarini, ndipo mwalimu wa zamu akatutangazia kuwa kuna wenzetu wamevamia shule ya wasichana na kushambulia walimu, hivyo uongozi umeamua kuwasimamisha masomo mpaka wizara itakapoamua vinginevyo.

Enzi hizo, uongozi wa shule haukuwa na mamlaka ya kufukuza mwanafunzi mpaka kesi ifike wizarani na ikijiridhisha, ndipo hatua zichukuliwe kulingana na uzito wa kosa. Bahati mbaya sana jamaa yangu alikuwa mmojawapo. Walifukuzwa hatimaye.

Sikushituka sana kusikia uhusika wake lakini nilijifikiria kuwa endapo nami ningekuwa kwenye msafara huo, ningekuwa mgeni wa nani kwenye familia yetu kwamba hata masomo ya kidato cha kwanza sijaanza nimetimuliwa! Nilimshukuru Mungu kwa kunichelewesha bwenini siku hiyo.

Kesho yake, Mkuu wa Shule akatutangazia rasmi uamuzi ule na kusema si rahisi shule kuvumilia kuishi na wanafunzi wa tabia kama ile wasioogopa kutoroka shule na kwenda shule nyingine tena ya wasichana, kufanya fujo ikiwa ni pamoja na kushambulia walimu.

Nimekumbuka tukio hili, kutokana na kauli zinazotolewa siku hizi na baadhi ya viongozi wa Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) bila hofu dhidi ya watu wengine wakiwamo wapinzani na hata viongozi wa juu wa serikali na CCM!


Nakumbuka tukio la kijana mmoja kuwasema viongozi wastaafu wa kitaifa eti wanaweweseka... eti wakae kimya kutokana na zama zao kupita, wasiharibu nchi na kumpotezea mwelekeo Mkuu wa Nchi na kwamba wakizidi watatwangwa!

Mwingine akaunganisha akisema badala ya kunyamazisha wapinzani kwa risasi watatumia sindano, huku akisisitiza kuwa serikali ya CCM haiwezi kupeleka maendeleo kwenye majimbo yanayoshikiliwa na wapinzani! Hata mwingine akamtishia maisha kiongozi wa upinzani kuwa angemmaliza.


Hivi karibuni, akaibuka mwingine akawaambia polisi wasijishughulishe kutafuta watu watakaopotezwa kwa kutukana viongozi. Maana yake ni kwamba watakuwa wameshauawa, hivyo polisi wafanye mengine na si kutafuta wendazao!

Hawa wana tofauti gani na wale jamaa zangu waliotoroka shule kwenda kufanya fujo shule nyingine tena ya wasichana, bila hata kutaka kuheshimu nafasi na hadhi za walimu wao? Leo tunashuhudia wapo wakidunda, wakibadilisha vituo vya kazi kama nguo. Mungu tuhurumie tu!

# MATUKIO KATIKA PICHA




Rais Samia Suluhu Hassan na Mgeni wake, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia, Dk. Hassan Sheikh Mohamud wakizungumza na waandishi wa habari, baada ya mkutano wao, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**




Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (kulia) akipokea mfano wa hundi ya sh. Milioni 20 kutoka kwa Ofisa Uhusiano wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Johary Kachwamba, mjini Kibaha juzi, kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko, katika wilaya za Rufiji na Kibiti. **PICHA: JULIETH MKIRERI**




Baadhi ya wakazi wa Kimara Suka, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, wakiangalia bajaji iliyopata ajari na kusababisha majeruhi ya watu kadhaa katika barabara ya Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Raia wa Kigeni kutoka China, wakichagua samaki aina ya Ngisi katika soko la Samaki la Kimataifa la Magogoni 'Feri', jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Baadhi ya wanachama wa Umoja wa Wakulima wa Chai (UWACHA) Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wakiweka saini kwenye azimio la kufungua akaunti iitwayo "Dunduliza Ropad" katika Benki ya NMB, wilayani humo, hivi karibuni, ili kuwa na mfuko wa maendeleo ya kilimo utakaofadhili kilimo hicho. **PICHA MPIGAPICHA WETU**


# MAISHA

APRILI 28, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14

## Utamu wa tembele



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Kitanda cha chuma nyumbani na faida zake



Ukurasa 12

**HARUSI**




## Pua inayong'ara

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | S | K | E | T | I |
| H | | | | L | | M |
| U | | B | E | E | | B |
| L | A | O | | Z | I | I |
| E | | M | B | A | | S |
| N | | B | | | | H |
| I | F | A | T | E | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

PAO, MEI, SAA, RAI, ELIMU, MKOSI, PEMBA, PIMBI, ABWAGWE, SHEREHE

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

WIKI HII TUNACHEMSHA AKILI KWA NAMBA. TAFUTA VIFUNGU VIFUATAVYO VYA NAMBA KATIKA JEDWARI HAPA CHINI. VIFUNGU HIVYO VIPO KUTOKA KUSHOTO KWENDA KULIA NA JUU KWENDA CHINI

6403 3683 3712 4800 8747 2675

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | 5 | 2 | 7 | 1 | 3 | 8 | 8 | 4 |
| 8 | 6 | 7 | 5 | 6 | 4 | 8 | 0 | 0 |
| 1 | 8 | 8 | 9 | 9 | 9 | 6 | 6 | 9 |
| 6 | 6 | 1 | 5 | 3 | 6 | 8 | 3 | 9 |
| 3 | 4 | 0 | 2 | 9 | 5 | 0 | 6 | 1 |
| 7 | 0 | 4 | 3 | 7 | 1 | 2 | 0 | 5 |
| 6 | 8 | 0 | 8 | 2 | 5 | 6 | 2 | 1 |
| 1 | 4 | 2 | 2 | 8 | 7 | 4 | 7 | 2 |
| 2 | 6 | 7 | 5 | 4 | 9 | 9 | 4 | 7 |

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kwa nini shetani anashambulia ndoa?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vituko katika duru la ndoa. Huko nyuma nilichambua maoni na madai ya baadhi ya kinababa wakilalamikia wake zao kuwakimbia, kisa mdororo wa kiuchumi.

Yaani maisha yalipokuwa mazuri walitulia, lakini uchumi wa mwanaume ulipoyumba, baadhi ya wanawake wakabwaga manyanga.

Je, ni utashi wao? Tokea mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, Mungu alikuwa amekusudia taasisi hii ya ndoa iwe yenye ushindi na mafanikio. Inahuzunisha leo kuwa watu wengi hawaoni ushindi huo.

Maandiko ya Mungu yanasema baada ya shetani kuingilia ratiba iliyokuwa imepangwa na Mungu, historia yote ya mwanadamu ilibadilika.

"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, ati, hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani?"

Hapa tunaona kwamba shetani hakumshambulia mwanaume moja kwa moja. Alikwenda moja kwa moja kwa mwanamke kwa sababu aligundua kuwa mwanamke alikuwa amepewa ngao ya kumlinda mwanaume. Alijua kuwa kama ngao ingetolewa mara moja, ingekuwa rahisi sana kumkamata Adamu.

> **UJINGA: Ujinga si tusi. Ujinga ni ile hali ya kutokwa na uwezo wa kufahamu jambo fulani, Ni ile hali ya kukosa maarifa kuhusu jambo.**

Maandiko yanaonyesha kuwa baada ya mazungumzo kati ya mwanamke (Hawa) na nyoka akimsisitiza kuwa akila matunda ya mti uliokatazwa hatakufa, ndipo akaingia kwenye mtego wa shetani.

Hawa hakuishia hapo, alikwenda kumshawishi na mumewe kula lile tunda. Na hicho kikawa chanzo cha mateso makubwa ya mwanadamu. Kilichotokea wakati ule ni zaidi ya anguko la Adamu na Hawa. Na kwa tukio hilo, ndicho chanzo cha vita kali kati ya mwanadamu na shetani.

Laiti kama yule mwanamke asingekuwa mjinga kumsikiliza shetani, katu shetani asingepata nafasi ya kutushambulia hivi leo.

Shetani na mawakala zake wamekuwa wakishambulia ndoa nyingi kwani leo hii ndoa hazina amani, furaha na upendo vimetoweka kwenye familia nyingi; mafarakano na chuki vimepandwa kwenye ndoa nyingi.

Swali la kujiuliza; kwa nini shetani amepata nafasi ya kushambulia ndoa leo? Ni ulweli usiopingika kuwa yule mwovu shetani amepata nafasi ya kushambulia ndoa nyingi na kusababisha ajali mbaya kwenye ndoa kwa sababu ya mambo mbalimbali. Hapa nitaje machache.

**UJINGA:** Ujinga si tusi. Ujinga ni ile hali ya kutokwa na uwezo wa kufahamu jambo fulani, Ni ile hali ya kukosa maarifa kuhusu jambo.

Mungu katika moja ya maandiko yake akasema, "Kwa sababu hiyo watu wangu wamechukuliwa mateka, kwa kukosa kuwa na maarifa na watu wao wenye cheo wana njaa, na wengi wao wanaona kiu sana." (Isaya 5:13).

Msomaji wangu, leo ndoa nyingi zinashambuliwa kwa kukosa maarifa. Ni maarifa tu ndiyo yanaweza kukutoa kwenye mateso ya ndoa unayopitia. Na ujinga ni moja ya silaha zenye nguvu anazotumia shetani. Ukitaka shetani aendelee kukutesa na kukuharibia maisha endelea kuwa mjinga.

Leo ndoa za Wakristo wengi zinashambuliwa kwa kukosa maarifa. Hivi unajua unaweza kuwa umeokoka kabisa na ni mwombaji mzuri lakini ndoa yako ikaangamizwa na shetani?

Hebu jiulize maswali yafuatayo;-

Je, una maarifa yapi kuhusu ndoa? Je, unapokutana na changamoto kwenye ndoa unapaswa ufanye nini? Je, wakati mumeo/mkeo amebadilika ghafla na kuwa mtu mwingine unatakiwa ufanyeje?

Pale unapogundua kuwa mumeo/mkeo ameanza kuwa na mahusiano na wanawake/wanaume wengine unatakiwa ufanyeje? Je, umesoma vitabu vingapi vya kiroho vinavyohusu ndoa? Ni maarifa tu yanayoweza kukusaidia kumshinda shetani na mawakala wake.

Sababu nyingine shetani kusambulia ndoa ni watu wengi kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ni muhimu kuzingatia kwamba kupata tu maarifa kuhusu ndoa haitoshi kumfanya shetani asikushambulie, bali kusimamia na kutendea kazi maarifa uliyo nayo.

Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa. Kwa bahati mbaya watu wengi walioko kwenye ndoa hupuuza na kutupilia mbali kanuni na maelekezo waliyopewa siku wanafunga ndoa.

Pale unapopuuzia kusoma vitabu vilivyoandikwa na watumishi wa Mungu kuhusu ndoa na jinsi ya kufanikisha ndoa yako, utajikuta unampa shetani nafasi ya kukushambulia.

Msomaji wangu naamini umejifunza kitu. Bado tunaedelea na uchambuzi huu na wiki ijayo tutaangalia zaidi chanzo cha matatizo ya ndoa.

**Je, una maoni au kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Wakili Minde umenena afya ya akili ni pasua kichwa

WANAHARAKATI ni sauti ya watu wasio na sauti. Wanaharakati hao wanaweza kuchochea mabadiliko makubwa ya mageuzi ya fikra, uchumi na mwenendo wa siasa za eneo fulani kama wanaona linalegalega na linahitaji ufumbuzi wa haraka.

Wana nafasi kubwa sana ya kuondoa mipaka kati ya rika, rangi, itikadi, jinsia na hali zote za kiuchumi.

Kwa nini naandika haya? Siku mbili zilizopita, nilimsikia mwanaharakati wa haki za binadamu na Wakili mkongwe nchini, Elizabeth Minde, akieleza kwa uchungu namna watoa huduma za kijamii hivi sasa wanavyoathirika kwa matatizo ya afya ya akili na trauma (kiwewe).

Mwanaharakati huyo anapigania watoa huduma wanaofanya kazi zinazofanana kama mashirika ya kiraia kusaidi wenye matatizo hayo, kupewa ujuzi wa kukabiliana na changamoto ya afya ya akili wakiwa katika mazingira ya kazi au nyumbani, ili kuhakikisha kupungua kwa matatizo hayo kwenye jamii, ambako inaonekana tatizo hilo limekithiri.

Anamaanisha kwamba matokeo ya matatizo ya afya ya akili na trauma hivi sasa, yanawaathiri wao na wateja wao.

Akashauri ifike mahali, serikali na wadau wake waje na mafunzo maalum, kwa sababu sasa yanaathiri na watoa huduma wanaoshughulika kila siku kupokea wateja mbalimbali kwenye masuala ya kisheria.

Minde anaamini kwamba kuwajengea uwezo kutasaidia kuangalia wanaharakati na afya zao za akili, na yale wanayokumbana nayo katika harakati, kuanzia familia zao, wanakutana na kesi ngapi na lipi suluhisho la afya zao za akili.

Nanukuuu: "Impact (matokeo) ya hivi vitu ni nini jamani, hata kwetu, inatuathiri sisi na wewe. Kwa hiyo lazima tujue namna ya kuhimili huo mlolongo inakuwaje, kwa sababu si tu tunazungumzia trauma ya mteja, tunazungumzia trauma ya watoa huduma pia.

"Unapozungumzia afya ya akili, wanakusimulia kama vile wewe ni kichaa, lakini ni kitu ambacho kinatokana na mwingiliano wa matatizo, inakuathiri wewe na inamuathiri na yule aliyekuja kwako, naye ameathirika vilevile.

Anakwenda mbali zaidi kwa kusema: "Mtu mwenye tatizo la afya ya akili, kwa mtu ambaye si mtaalamu anatakiwa amuonyeshe sehemu ya kwenda au kumpatia ushauri wa awali, na kwa mtu ambaye ni mtaalamu, anatakiwa kumshauri na kumfanyia rufaa kwa wataalamu wengine,maana changamoto hii ina athiri wakati mwingine hadi mwili."

> **Anamaanisha kwamba matokeo ya matatizo ya afya ya akili na trauma hivi sasa, yanawaathiri wao na wateja wao.**

Niliposikia maneno hayo ya Wakili Minde, nilimtafuta haraka haraka, rafiki yangu, Daktari Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Editruda Gamassa, nikamshirikisha kuhusu hayo yanayozungumzwa na wanaharakati.

Alinijibu kwa kifupi tu kwamba magonjwa ya afya ya akili ni matatizo ya ubongo ambayo humfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii.

Pasina shaka kwamba ni kawaida kuwa na hisia kali, kutokana na tukio la kufadhaisha au la kuogofya.

Dk. Gamassa akaniambie tena, kwamba ni kawaida kuwa na miitikio mikali ya kihisia au kimwili. Kwamba, watu wanaweza kupata aina mbalimbali za athari za kimwili, kiakili, kihisia na kitabia.

Kitaalam anasema tukio la kiwewe ni tukio lolote maishani ambalo husababisha tishio kwa usalama wetu na kuwezekana kuweka maisha yetu au ya wengine hatarini.

Kwa hiyo, mtu hupata viwango vya juu vya dhiki ya kihisia, kisaikolojia, na kimwili ambayo huvuruga kwa muda uwezo wake wa kufanya shughuli kwa kawaida katika maisha ya kila siku.

Mifano ya matukio yanayoweza kuhuzunisha ni pamoja na misiba ya asili, kama vile mafuriko, kupata ajali mbaya ya gari, kuwa ndani ya ndege ambayo inalazimika kutua kwa dharura, au kushambuliwa kimwili.

Licha ya kuwapo mambo mengi unayoweza kuyafanya ili kukabiliana nayo na kupona kiwewe, baada ya kupata msaada wa kitaalamu ili kuanza kurudi katika hali ya kawaida.

Walakini mara nyingi, athari hizi hupungua kama sehemu ya mchakato wa uponyaji wa asili wa mwili na kuzoea.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 715 545 490**

# HARUSI









Hakika ni kumbukumbu iliyotukuka kwa Amani Magelanga na mkewe Anna Siwonike wakati walipofunga ndoa Desemba 4, 2021 katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya Iringa.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# Fulana ya mikono mirefu, wengi hawajui kuchagua



WAKATI vazi la fulana la mikono mirefu limekuwa likipendwa na wanaume, bado wamekuwa na mapungufu ya namna ya kuchagua na kuvaa.

Wataalamu wa masuala ya mavazi wanasema fulana ya mikono mirefu yanahitaji umakini katika kuchagua na kuvaa ili kupata matokeo mazuri.

Haya ni baadhi ya mambo unayotakiwa kuyafuata ikiwa unahitaji kuvaa fulana ya mikono mirefu.

**CHAGUO BINAFSI**

Je, wewe ni aina ya mtu ambaye unapenda starehe badala ya mtindo? Au wewe ni mtu ambaye unapenda kuhusisha mitindo ya kisasa? Hayo ni maswali unatakiwa kujiulia na kupata jibu sahihi ili kujua wewe unafaa kuvaa auna hii ya fulana.

Ikiwa huwezi kutambua kile unachopenda sana, mpe rafiki yako nafasi ya akuchagulie au jaribu kuvaa fulana chache utakazozinunua.

**UMBO LAKO**

Kosa kubwa ambalo wanaume hufanya wakati wa kuchagua nguo hizi ni kutozingatia jinsi miili yao inavyojengwa.

Aina ya umbo sio kwa wanawake pekee, bali hata kwa wanaume kwani ni kitu muhimu ili kupata nguo yenye ukubwa na urefu sahihi.

Kama hauwezi kutambua umbo lako, jaribu kumuuliza mtu mwenye ufahamu kuhusu mitindo akupe usaidizi.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# PUA INAYONG'ARA

RANGI nyeupe inayoonekana juu ya pua ni dalili kuwa kuna gozi iliyokufa ambayo imekutana na pua na kusababisha vipele vidogo.

Vipele hivyo ni aina ya chunusi na huwatokea zaidi watu wenye ngozi za mafuta kwa wanawake na wanaume.

Unaweza kuziondoa chunusi hizo kwa njia za asili ambazo kila mtu anaweza kufanya akiwa nyumbani kwake.

Unachotakiwa ni kuosha uso wako mara mbili kwa siku na maji ya uvuguvugu.

Baada ya kuosha fanya kama unapigapiga taulo usoni usisugue. Hii ni njia inayopunguza uchafu na mafuta kujijenga kwenye mashimo ya ngozi.

Steaming ni njia nzuri ya kuondoa vipele, unachotakiwa kufanya ni kuchemsha maji kisha uyamimine kwenye bakuli.

Acha ule mvuke ukupige usoni kwa muda wa robo saa. Hii ni njia nzuri ya kufungua tundu au vinyweleo kwenye ngozi ambapo inakuwa rahisi kuondoa uchafu kwenye ngozi.



Ukitoka kuoga, tumia vidole vyako viwili kusugua taratibu eneo la pua, itaondoa ngozi zote zilizokauka.


Epuka kujishika eneo hilo wakati wote kwa sababu vijidudu vilivyopo kwenye mikono vinasababisha hali hiyo kuendelea au kuongezeka.


Unaweza kutumia njia nyingine ukiwa nyumbani kuondoa vipele hivyo.

Pia njia nyingine ni kutumia majani shubiri (Aloevera), mti huu unaua vijidudu kwa kiwango kikubwa.

Changanya matone matatu ya juisi ya limau na jeli ya Aloe vera. Weka kwenye uso, kisha sugua taratibu kwa robo saa. Baadaye safisha uso kwa kutumia maji moto.

Nyanya ni tiba nzuri ya kutibu tatizo hili. Chukua juisi ya nyanya na upake usoni na kaa hadi ikauke. Kisha osha uso kwa maji ya uvuguvugu.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa tembele

TEMBELE ni aina ya mboga inayopendwa na idadi kubwa ya watu, lakini inachukuliwa kama chakula kinacholiwa na wasio nacho.

Wasichojua ni kwamba ni mboga inayotia hamu na tamu kama utaipika vizuri.

Tuangalie kwanza maandalizi yake na namna ya kupika mboga hii inayonoga zaidi kula kwa ugali.

**Mahitaji**

Tembele lenyewe kiasi cha fungu moja, nyanya tatu zilizoiva vizuri, kitunguu maji, chumvi, mafuta ya kupikia na limao au ndimu ya maji.

**Mapishi**

Kwanza chambua vizuri tembele lako, kisha osha vizuri na anika kidogo lichuje maji. Kuna wengine wanapenda kupika moja kwa moja baada ya kuosha bila kuanika.



Weka sufuria au chungu motoni, weka mafuta ya kutosha, maana tembele linahitaji mafuta la sivyo utalichukia na ndio sababu wengi hulalamika matembele sio mazuri, kumbe wanapunja mafuta.

Tia kitunguu geuza geuza kisha tia nyanya zako na chumvi kidogo.

Nyanya zikiiva weka tembele lako. Ligeuze hapo mpaka linywee weka maji kidogo sana kisha funika kidogo.

Unatakiwa ukae huku ukiangalia kama limeiva. Ukiona bado ongeza maji kidogo usiweke maji mengi unaweza kuharibu ladha.

Mwisho kamulia kipande cha ndimu au limau geuza dakika mbili hadi tatu, hapo tayari kwa kula kwa ugali wako wa moto.

MAISHA NI NYUMBA
Na Restuta James

# Tairi chakavu katika pambo

KILA kitu kinaweza kubadilishwa na kutumiwa kubadili mwonekano wa bustani au nyumba yako, ni kiasi cha namna mtu anavyotazama vitu.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kila kitu kinafaa kubadilishwa, safari hii wakizungumzia matumizi ya tairi chakavu kama moja ya zana za kubadili mwonekano wa nyumba.

Wanaeleza kuwa tairi hizo zinaweza kupakwa rangi nyeupe, nyekundu, njano, bluu, pinki, kijani au nyeusi kulingana na mapenzi ya rangi kwa mwenye nyumba.

Aidha, tairi hizo zinaweza kupakwa rangi za aina tatu na kuongeza nakshi stahiki. Hata hivyo, wanaeleza kuwa inategemea ni wapi hasa mtumiaji anapanga kuziweka kama ni chini au kuning'iniza.

Wanaeleza kuwa tairi zinaweza kutumika kama chombo cha kupandia maua nje ya ukuta, kutengeneza fasheni ya mzunguko (round about) au ngazi kwenye bustani.

Pia wanaeleza kuwa tairi zinaweza kuning'inizwa ukutani kwa kushikiliwa na msumari au kifaa kingine kitakachopatikana kwa urahisi.

Rangi zinazoshauriwa kupakwa kwenye aina hii ya pambo ni zile angavu kama pinki, njano, bluu bahari, nyekundu na nyeupe. Hii ni kwa sababu maua mengi yanatawaliwa na rangi ya kijani hivyo kupaka rangi hizo kutaongeza mwonekano mzuri zaidi.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, si maua pekee unayoweza kupanda kwenye tairi bali unaweza kuzitumia kutengeneza bustani yako ndogo ya mboga mboga nyumbani.



Na Elizabeth Zaya









# Kitanda cha chuma nyumbani na faida zake

MOJA kati ya mambo muhimu kununua ambayo mtu hufanya katika nyumba yake ni kitanda kutokana na umuhimu wake hasa kwa kupumzisha mwili baada ya shughuli za kutwa nzima.

Kitanda cha chuma nacho kinapowekwa kwenye chumba, kina mvuto wake kwenye nyumba.

Mbali na kuleta mvuto kwenye chumba, Erick Fabian, ambaye ni mtengenezaji wa vitanda vya chuma katika eneo la Mbezi Makonde, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, anaeleza faida na hasara za kutumia kitanda hicho.

Kwa upande wa faida, anasema kitanda cha chuma ni imara na kina uwezo wa kudumu kwa muda mrefu.

Faida nyingine, anasema kina uwezo wa kuhimili uchakavu na hakiharibiki kirahisi hata pale kinapokuwa kimetengenezwa kwa mtindo wa kubebana juu na chini (deka).

Kwa mujibu wa Fabian, faida nyingine ni kwamba kitanda hicho ni chepesi kulinganisha na cha mbao ngumu na kwamba ni rahisi kukipangilia kwenye chumba namna unavyotaka.

> **Kwa upande wa faida, anasema kitanda cha chuma ni imara na kina uwezo wa kudumu kwa muda mrefu.**

Anasema hata unapotaka kukifungua kwa ajili ya kukisafisha kwa ndani zaidi au kwa kuhamishia katika chumba kingine, hakisumbui kwa sababu ni rahisi kukifungua.

Pia anasema kitanda cha chuma kina matumizi madogo ya eneo la chumba kwenye nyumba kwa sababu miguu yake ni myembamba tofauti na ilivyo kwa kitanda cha mbao.


Sambamba na hilo, anasema kwa kawaida kitanda cha chuma kimepanda juu, hivyo kinampa msafishaji urahisi wa kufanya usafi hadi chini ya uvungu.

Kuhusu hasara zinazotokana na kitanda cha chuma kwenye nyumba, anasema ni kuharibika kwa mipira inayokuwa imewekwa kwenye miguu inayokishikilia ambayo inaposagika na isipobadilishwa kwa haraka huharibu sakafu hasa pale kinaposogezwa.

Anasema kitanda hicho kina kawaida ya kubadilika kuendana na hali ya joto au baridi endapo chumba kikipata baridi au joto, huwa vivyo hivyo kwa kitanda kuwa na joto au baridi katika nyakati za baridi na pia kitanda hicho husika kutu.

"Kitanda cha chuma kinaweza kisiwafae watu wa mabondeni ambao nyumba zao zinatuama maji sakafuni kwa sababu endapo maji yatatuama kwenye chumba kwa zaidi ya siku tatu, kuna uwezekano mkubwa wa kutoba sakafu na kutumbukia ndani kidogo kidogo. Lakini pia miguu ya kitanda inaweza kuharibiwa na kutu," anasema.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
TULIKUTANA NA MKE WANGU KWENYE KLINIKI YA 'MAMBO YETU YA DOZ' MREMBO WA KUVUTIA KAMA MALAIKA
ULITAKIWA KUSEMA MAPEMA WAKATI UNANIKABIDHI FAMILIA YAKO NILIPOKUPA SAFARI YA KIKAZI... SA'ITAKUAJE!
JUKWAANI
TWENDE HUKU UKAMALIZIE 'VIPORO' VYAKO NDIO UJIANDAE KUOMBA KURA ZETU UCHAGUZI UJAO
HIVYO VIPORO NI CHAMBO CHA KUOMBEA KURA NIMEVIACHA MAKUSUDI
MBONA NAJIONEA MALIMWENGU LAIVU! UMEFUNGA SAFARI KUJA KUOMBA NIKUTENGENEZE UPUNGUZIWE MSHAHARA BADALA KUONGEZWA? UPO SILIAS?
MSHAHARA NI MKUBWA NIKIUPOKEA TU, LAZIMA NIANZE MSAKO WA JIMBO JIPYA MPAKA NILIPATE! KISHA NAKITA KAMBI YA MUDA!
USINIZUGE! MPIRA GANI NA MANUNDU KAMA UMENG'ATWA NA NYUKI?
WE' UNADHANI MASHABIKI WANA JEMA? FANYA VIZURI MARA MIA, ALAFU KOSEA MARA MOJA UONE!

HABARI KIMATAIFA

# Rai Biden akubali mdahalo na Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema yuko tayari kupambana na mgombea mtarajiwa wa urais kupitia chama cha Republican Donald Trump, kwenye mdahalo.

Rais Biden ametoa matamshi hayo alipoulizwa na mtangazaji wa kituo cha Radio cha XM, Howard Stern kama yuko tayari kushiriki mdahalo huo na Trump utakaoandaliwa kabla ya uchaguzi.

Hadi sasa, timu ya kampeni ya Biden bado haijazungumzia chochote kuhusiana na suala la kiongozi huyo kushiriki kwenye mdahalo huo.

Hata hivyo, Machi mwaka huu Rais Biden alisema ushiriki wake utategemea na tabia za Trump.

"Nitafurahi kupambana naye, ninajiandaa na sijui ni lini," Biden alijibu kwa bashasha. Trump ambaye tayari alikubali kupambana kwenye mdahalo na Biden, hata hivyo ametilia mashaka utayari huo wa mpinzani wake.

Kiongozi huyo wa zanmani wa taifa hilo kubwa, alisisitiza tena kwamba yuko tayari kwa mdahalo huo mahali popote na wakati wowote.

Trump anamshutumu Biden kwa kutumia mfumo wa haki kuhujumu jitihada yake ya kurejea Ikulu ya White House, alipendekeza kufanyika kwa mjadala huo katika mikutano yake ya kampeni katika jimbo la Michigan wiki ijayo.

Kwenye mtandao wake wa kijamii wa Truth, Trump alilalamika "Nimekwama kwenye moja ya kesi nyingi zilizoko mahakamani dhidi yangu ambazo Biden alizianzisha ili kuingilia uchaguzi dhidi ya mpinzani wake wa kisiasa."

Rais Biden na Trump walikutana kwenye midahalo miwili wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Midahalo ya wagombea huwa ni hatua kubwa na ya muhimu katika mchakato wa uchaguzi mkuu nchini Marekani kwa miaka mingi, ikilenga kuwasaidia wapiga kura kuwatathmini wagombea.

Biden ambaye anamtaja Trump kama kitisho cha demokrasia aliwaambia waandishi wa habari mwezi uliopita kwamba makubaliano yoyote ya mdahalo yanategemea tabia yake.

**DW**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken akikaribishwa na Rais wa China, Xi Jinping katika ukumbi mjini Beijing, juzi. **PICHA:REUTERS**

# Marekani kupeleka makombora Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

WIZARA ya Ulinzi ya Marekani, imetangaza kuharakisha kupeleka makombora ya ulinzi wa anga ya Patriot na risasi za kivita nchini Ukraine kama sehemu ya kifurushi chake kipya cha msaada wa kijeshi.

Kulingana na Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo, Lloyd Austin, mifumo ya Patriot ya kurusha makombora haitapelekwa nchini humo.

Kwa upande wa Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alisema makombora ya Patriot yanahitajika haraka kukabiliana na tishio la anga kutoka kwa Russia na Marekani inapaswa kuokoa maisha ya watu haraka iwezekanavyo.

Serikali ya Ukraine ilisema jana Russia ilifanya shambulio lingine kubwa la anga na kuharibu hospitali moja.

Pia miundo mbinu ya nishati katika mikoa mitatu ilishambuliwa.

Russia ilishambulia kwa makombora kutoka kwenye meli aina ya S-300, ardhini na angani kwa kutumia makombora ya balestiki ya Iskander.

Katika makombora hayo 21 yaliangushwa kwa kutumia ndege na mifumo ya ulinzi wa anga.

Ukraine nayo ilidai kushambulia vinu viwili vya mafuta vya Russia upande wa pili wa mpaka.

Picha kutoka moja katika eneo la Krasnodar ilionekana kusababisha mlipuko mkubwa, ingawa viongozi wa eneo hilo walikanusha uharibifu huo.

Mamlaka ya Russia ilisema kuwa iliangusha ndege 68 zisizo na rubani za Ukraine katika eneo hilo.

**BBC**

# Mapigano yazidi kuongezeka Ukanda wa Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MAPIGANO yanazidi kuenea katika eneo la Mashariki ya Kati baada ya Israel kushambulia mashariki mwa nchi ya Lebanon jana.

Aidha, vikosi vya jeshi la Israel bado vinashambulia kwa mabomu maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Gaza na hasa katika mji wa Rafah ulioko kusini mwa nchi hiyo. Wakazi wameripoti kuwepo kwa shambulio jana usiku, Saa chache kabla wajumbe kutoka nchini Misri kuwasili Israel kujaribu kuanzisha upya mchakato wa mazungumzo.

Kundi la Hamas linalotawala Gaza lilitangaza jana kwamba linatathmini pendekezo la Israeli linalopinga usitishwaji vita kujaribu kufikia makubaliano na kuachiliwa kwa mateka wa Israeli.

Majadiliano hayo yanahusu muda wa kusitisha mapigano, kuondolewa kwa jeshi la Israel kutoka eneo lote au sehemu ya Ukanda wa Gaza, kurejea kwa Wapalestina waliokimbia katika maeneo yao ya asili na kuachiwa kwa misaada ya kibinadamu.

Pia majadiliano hayo yatajikita kuangalia idadi ya mateka wa Israel walioachiliwa katika makubaliano ya awali.

Kwa upande wa Israel, ikikubali mapatano ya kutaka kuachiliwa kwa mateka wa Hamas au kuanzisha operesheni ya kijeshi ya ardhini huko Rafah kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Serikali ya Israel imekuwa ikisimama katika njia panda kwa wiki kadhaa bila ya kuchagua mwelekeo ambao nchi itachukuwa.

Wakati huo huo, maelfu ya Waisraeli wataandamana tena kutaka kuachiliwa kwa mateka na kutaka serikali ijiuzulu au madai yote mawili yatekelezwe.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Stéphane Séjourné, yuko Mashariki ya Kati kuzuru nchi za Israel, Palestina na Saudi Arabia.

Lengo la ziara hiyo ya kidiplomasia ya Ufaransa ni kuepusha mapigano kwenye mpaka kati ya Lebanon na Israeli.

**RFI**

# Mafuriko yaua watu 70 Kenya

**NAIROBI,** KENYA

MAFURIKO yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini Kenya, yamesababisha vifo vya watu 70 kuanzia katikati mwa mwezi uliopita.

Hayo yameelezwa na msemaji wa serikali, Isaac Mwaura, akisema ni mara mbili ya idadi iliyoripotiwa wiki hii.

Hata hivyo Mwaura, alikanusha madai kwamba mamia ya watu wamekufa kufuatia mafuriko hayo yanayoendelea kuikumba nchi hiyo.

Kwa wiki kadhaa sasa, nchi hiyo ya Afrika Mashariki imekuwa ikishuhudia mvua nyingi inayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

MAKALA

# ELIMU PEKEE BILA AKILI, HATUTAFANIKIWA



Na Magabilo Masambu

**Kila anayesoma anatarajia mafanikio yatokanayo na elimu yake. Hata hivyo, lazima tufahamu kwamba kuwa na elimu pekee bila akili hatutafanikiwa. Lazima tuwe na akili ya kubuni namna ya kutatua changamoto zinazotuzunguka bila kujali tuna elimu kubwa kiasi gani.**

MWANASAYANSI mashuhuri, Albert Einstein, alipoulizwa akili ni nini, alisema "akili ni kile kinachobakia baada ya kuondoa yote uliyofundishwa darasani".

Kwa mujibu wa Einstein, unaweza ukawa na elimu ukakosa akili. Vilevile unaweza ukawa na akili ukawa umekosa elimu na kwamba akili ndiyo ilibuni elimu. Yaani watu wenye akili walikaa wakaweka utaratibu wa mtu kukaa darasani na kujifunza kwa kipindi fulani, kisha apimwe kwa mitihani na atunukiwe cheti. Ubunifu huo ulifanywa na wenye akili.

Ni ukweli kwamba dunia imeendelea kuwa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa sababu ongezeko la watu haliendani na miundombinu yenye kutoa fursa za ajira.

Hii inamaanisha kuwa hatuwezi kuajiriwa wote, hivyo lazima tuwe na watu wenye akili watakaobuni shughuli ambazo zitaajiri wenye elimu.

Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, katika kitabu chake cha Elimu ya Kujitegemea, anasema watu wengi wanatafuta elimu si kwa ajili ya kutafuta maarifa yawasaidie kutatua matatizo yao ya kila siku, bali wanasoma sana ili kujaribu kuyakwepa matatizo yenyewe.

Yaani mwenye diploma anasoma digirii akiamini kwamba kwa kuipata digirii atakuwa amepunguza shida kwa kutegemea kipato kikubwa.

Vivyo hivyo, kwenye ngazi nyinginezo za juu kabisa kuufikia uprofesa lakini bado maisha husalia yakiwa ya kuhangaika.

Lengo la elimu si kuipata ili kukwepa matatizo bali kuitumia kutatua matatizo. Kama utakuwa na elimu ikashindwa kutatua changamoto zinazokukabili au zinazoikabili jamii, basi unaweza kuwa na elimu ukawa umekosa akili.

Tatizo kubwa tulilo nalo ni kubeba elimu zetu na mwisho tunazeeka bila mali.

Baadhi ya wenye elimu hudhani kwamba elimu zao ni kinga katika kujishughulisha na baadhi ya shughuli ambazo hufanywa na wenye akili wasio na elimu! Kumbe ni bora ukakosa elimu ukawa na akili, hivyo unaweza kupata mali.

Uzoefu unaonyesha kwamba wenye elimu wengi wameajiriwa na wenye akili, yaani wasio na elimu ya darasani.

Wakati huo huo, wenye elimu wamebaki kujisifu kuwa na vyeti vizuri bila mali. Tutaanza kuendelea tu pale tutakapokubali kwamba elimu zetu si kitu bali tunapaswa kutumia akili ili tupate mafanikio ya kimaisha.

Kwa mujibu wa kitabu cha Mkurugenzi wa Chuo cha Habari cha Fanikiwa kilichoko Arusha, Joseph Mayagira kiitwacho "KUBUNI BIASHARA IKUPASAYO", mambo matano yanatakiwa ili ili kufanikiwa kibiashara. Jambo mojawapo anasema: "Ili kufanikiwa kiuchumi ni lazima kubuni kitu cha thamani kwa maisha ya watu."

Hapa inahitajika akili kufahamu kwamba jamii ina changamoto gani ili kubuni biashara itakayotatua changamoto hiyo.

Kila anayesoma anatarajia mafanikio yatokanayo na elimu yake. Hata hivyo, lazima tufahamu kwamba kuwa na elimu pekee bila akili hatutafanikiwa. Lazima tuwe na akili ya kubuni namna ya kutatua changamoto zinazotuzunguka bila kujali tuna elimu kubwa kiasi gani.

Baadhi ya wanaojiita wasomi wamesikika mara kadhaa wakisema hawawezi kufanya hiki na kile kwa kuwa wana elimu kubwa. Wengine wamekuwa wakikataa kuajiriwa kwa kuwa wanaona watalipwa ujira mdogo, huku wakiamini wana elimu kubwa bila kufahamu kwamba mwanzo wa kuwa na kikubwa ni kuanza na kidogo ili kujitengenezea mazingira ya kupata kikubwa, hivyo hubaki bila ajira.

Tofauti kati ya wenye akili na wenye elimu ni kwamba wenye elimu kila tunalofanya lazima wahusishe na elimu yao.

Lakini ni muhimu kufahamu kwamba mfumo wetu wa elimu kwa kiasi kikubwa hauendani na mazingira tuliyo nayo.

Mfano unakuta tunajifunza jinsi wakoloni walivyotumia njia mbalimbali kututawala na tunafika vyuo vikuu kwa kufahamu vyema kueleza vizuri njia hizo.

Lakini uhalisia wa maisha katika kufanikiwa, hiyo ina maana gani hasa? Kama tunataka kufanikiwa kwa kutumia elimu zetu, lazima tukubali kwanza kubadili aina ya elimu tuliyo nayo kisha tuitumie katika mazingira yetu.

Limekuwa jambo la kawaida kwa kijana aliyekulia kijijini akifanya shughuli za kilimo baadaye akaenda chuo kikuu na baada ya masomo, anaona si halali tena kwake kufanya kilimo.

Anaona kilimo si hadhi yake kwa maana sasa ni msomi! Anapewa heshima kiasi kwamba hata wazazi wanaogopa kumtuma kazi zile alizokuwa akizifanya kabla ya kufika chuo kikuu.

Tukibadili mtazamo tutabadili maisha, elimu iwe nyenzo ya kutuongezea ufahamu tu lakini lisiwe tegemeo la kutupatia ajira. Vinginevyo iwe imebedilika kiasi cha kuwafanya wanafunzi kuwa wabunifu kufanya shughuli zenye kutatua matatizo mabalimbali kwenye jamii.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mama ana makosa, nifanye nini? Baba mgomvi, niamuaje?*



Na Adam Fungamwango

WAKO baadhi ya watu ambao maisha waliyonayo sasa yametokana na ugomvi wa wazazi wao. Wazazi waligombana, wakaachana, wakagawana watoto, au wakabaki kwa mmoja wao.

Wakati mwingine maisha yanakwenda kama yalivyopangwa, lakini kuna wakati watoto wanakumbana na hali ngumu ya mateso kutoka kwa mama au baba wa kambo.

Hawa ni wale walezi wanaoishi na mmoja wa wazazi wao. Baadhi yao hawawapendi, au hawataki kuwapa malezi sawa kama watoto waliowazaa.

Matokeo yake watoto wanakosa malezi mema, elimu bora na inafika wakati watoto wanaamua kuondoka nyumbani mapema ili kujitafutia maisha hata kama yatakuwa duni, ili mradi tu kuepukana na dhahama wanayoipata nyumbani.

Ukiacha hilo, kuna watoto wanaokutana na changamoto ya kuona wazazi wao wanagombana mara kwa mara nyumbani. Hawa huwa hawaachani, lakini nyumbani kuna hakuna amani. Kila siku wazee, majirani na ndugu wanaosuluhisha.

Katika hili, watoto badala ya kusimama katikati, wanachukua upande. Mara nyingi inakuwa kwa mama. Imezoeleka tu na watoto au jamii kudhani unapotokea ugomvi, au kutokuelewana baina ya mke na mume, basi mwanaume ndiye moja kwa moja ana makosa.

Hii inawafanya wanaume wengi kuwa wanyonge, au kuwa wakatili kupita kiasi kutokana na kuonekana kama hawasikilizwi na watoto wala jamii.

Wakati miwngine hii inatokana na tabia ya wanaume wenyewe kutopenda kuweka sababu za mgogoro wake na mkewe hadharani. Hii kuwa inawagharimu sana.

Mwanamke atakusanya watoto na kuwaambia, "baba yenu siku hizi amebadilika, hata mnaona kula imekuwa ya shida, ada imekuwa matatizo kwa sababu ana nyumba ndogo.

Yule Amina mnayemwona nyumba ya mtaa wa pili pale, ni mama yenu mdogo, pesa zote zinaishia kwake" na maneno mengi ambayo yanawaingia watoto na kuanza kumchukia baba yao.

Sasa kuna wale ambao wakishakuwa wakubwa wanaanza kuona ukweli wenyewe na kuona baba yao hakuwa na kosa, lakini wengi wanaendelea kuwa upande wa mama, kiasi kwamba mzee hata akistaafu na kukaa nyumbani, bado hapati upendo kwa watoto wake kama wanaoutoa kwa mama yao. Sina uhakika, inawezekana hii ikawa moja ya sababu nyingi zinazowafanya wanaume kufa mapema. Wanakuwa wapweke katika jamii hadi kwenye familia zao mwenyewe.

Wanaume hata wakifanyiwa visa na vituko vipi, lakini sijui kwa nini. Huwezi kukuta kakusanya watoto wake anawaambia matatizo ya mama yao moja baada ya jingine. Mara nyingi utasikia wakiwaambia, "haya ni matatizo yetu, nyinyi bado wadogo sana, mkikua mtayaona."

Mwanamuziki Cosmas Thobias Chidumule, enzi za miaka ya 1980, akiwa na bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra, alikutana na changamoto hiyo ya wazazi wake. Akatunga vibao viwili vinavyozungumzia mgogoro wa wazazi wake, akaviuta, 'Barua Kutoka Kwa Mama'sehemu ya kwanza na ya pili.

Chidumule ambaye kwa sasa anaimba nyimbo za injili, katika wimbo wa sehemu ya pili, anawaasa watoto kutoegemea upande wowote wa wazazi iwapo kutakuwa na mgogoro. Na anashauri ni bora kuita watu wengine kuusuluhisha, lakini wao wasijihusishe kabisa kwa sababu wote ni wazazi, huwezi kumwambia mmoja kuwa ana makosa. Anatolea mfano wa yeye mwenyewe kilichomkuta na alichoamua. Wimbo ni huu hapa.

"Ugomvi wa baba na mama, siwezi kuingilia kwa sababu ningali mdogo wapo wazee, majirani na ndugu watakaosuluhisha, ohohohohoo.

Ingawa rafiki zangu wananilaumu, eti siwajali wazazi wangu, tena siwajali kwa shida na mambo yao, siyo kweli mimi nasema, ukweli ninao mwenyewe heeee, nitawaeleza.

"Nakumbuka miaka ya nyuma, nilipopokea barua kutoka kwa mama, akinipa malalamiko yake, kwamba yupo mbali baba, mamaaa.

Kwa uchungu niliijibu barua ya mama, ya kwamba nitajaribu kuyasuluhisha, lakini mimi nilishindwa leo, nawaeleza muelewe jamani ee, sitaki mnilaumu mie mwenzenu ee, matatizo yamenizidi umri eee, nataka mjue.

"Aaaaa, yoooo malalamiko yenu, yeeeee mnayonilaumu, nataka muyaache.

Hata kama mama ndiye mwenye kosa nifanye nini, hata kama baba ndiye mwenye kosa niamueje miye. Nisijekosa radhi ya baba, nisijekosa radhi ya mama.

"Matatizo, kila mtu anayo, mengine hufanana na mengine hutofautiana. Na hata jinsi ya kuyatatua hutofautiana, hebu jamani nipeni busara zenu nifanye nini miye oooo, nisije nikaharibikiwa woo.

"Naepuka lawama, naepuka lawama mimi siyo mtoto upande mmoja nisimame upande gani mwenzenu, hebu jamani nambieni ili nisijekosa radhi ya baba au mama, kwani wazazi duniani ndiyo kitu cha kwanza, elewa ee, ninayosema wowooo.

"Hata kama mama ndiye mwenye kosa nifanye nini, hata kama baba ndiye mwenye kosa niamueje miye. Nisijekosa radhi ya baba, nisijekosa radhi ya mama."

Watoto chukueni somo la Chidumule, msiegemee upande mmoja.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKAWAZA kitu kingine kabisa. Akatabasamu. “Ndiyo, hapa sasa tatizo litakuwa limeisha.” Akajisemea mwenyewe huku akipiga ngumi za ushindi hewani.

Presha ikamshuka, furaha ya kutembelewa na mpenzi ikarejea tena. Mwanzoni aliona dakika chache tu zimebaki kabla hajafika, lakini kwa sasa aliziona ni nyingi.

Wazo la kumsaka panya aliyekufa likafa kabisa. Kwa sababu ameshafanya hivyo zaidi ya saa mbili bila mafanikio. Sasa alikuwa na wazo la njia mbadala ili kupoteza harufu ya panya ili isimkere mgeni wake.

Hapo Alikuwa na uhakika kitu alichokiwaza kukifanya ili kupoteza harufu ya panya kitafanikiwa na ilikuwa ndiyo njie pekee iliyobaki kwa muda huo. Akachukua shilingi elfu moja iliyokuwa mezani, akaiweka kwenye mfuko wake na pensi aliyovaa.

Akaangalia tena saa yake, zilibaki dakika 15 tu. Tayari kwake zilikuwa nyingi hata akifikiria mara nyingi kuna ahadi zinazoitwa za kiswahili. Alijua huenda kuna dakika tano au 10 zingine za ziada kabla mgeni wake hajaingia. Zilitosha kabisa kutoka na kwenda kuchukua kitu ambacho aliamini ndiyo mwarobaini ya harufu hiyo ya panya chumbani mwake.

Alirejea baada ya 10 kupita. Sasa zilibaki dakika tano peke yake kufika saa 10:00 jioni, muda ambao Nuru aliahidi angefika.

Hakuwa na wasiwasi tena, alianza kupiga mluzi, huku akitafuta kibiriti. Alikwenda kwenye meza yake ambayo ina jiko la mchina kuangalia pembeni yake kama anaweza kuona kibiriti. Alikumbuka kuwa juzi alikinunua. Hakukiona, ikabidi aangalie chini.

Akaona ganda, moyo wake ukajaa amani. Kumbe kilikuwa kimeanguka chini yeye hana habari.

Alipokiota kwanza alikitingisha, uzito wake jinsi sauti yake ilivyosikika kilionekana kuna njiti chache sana.

Akakifungua.

Ni kweli zilibaki njiti tano tu. Sasa kazi iliyokuwa nayo ni kuwa mwangalifu ili zisizime kabla ya kitu anachotaka kuwasha kuwaka. Na kweli ikawa hivyo.

Njiti tatu zote zilizimika, zikabaki mbili tu. Akaona huenda anaweza kuwa na kazi nyingine ya kurudi tena dukani kununua kibiriti wakati muda tayari umekwisha.




**Baada ya kupata vipimo na kupata nafuu na kuwa na hamu ya kula alikwenda kuagiza supu ya utumbo na chapati mbili wakati haikuwa kawaida yake. Kwa sababu chapati zilikuwa bado zinachomwa, alielekeza kama ikiwa tayari aletewe nyumba ya tatu kutoka wanapouzia, pamoja na chumba anachoishi cha uani.**

Akaangalia saa zilibaki dakika mbili tu. Akawaza safari ya kwenda dukani mpaka kurudi tena anaweza kutumia dakika 10 zingine.

Kwa uangalifu mkubwa, akachukua njiti ya nne, akasongea sehemu ambayo aliamini kuna upungufu wa upepo ambao unaweza kuzima kibiriti alichowasha.

Akawasha, kibiriti kikawaka, haraka alichofanya ni kuchokua kitu alichonunua na kukiunganisha na moto uliokuwa unawaka kwenye njiti. Kikawaka. Tayari ilibaki njiti moja kwenye ganda.

Alikuwa amefamikiwa. Akashusha pumzi. “Kazi imekwisha.” Akajiambia mwenyewe.

Kitu alichokwenda kukunua hakikuwa kingine bali ni udi.Hutumika kutoa harufu nzuri ya marashi chumbani, na sehemu nyingine mbalimbali kama za biashara, na zingine zinazofanana na hizo. Wengine hujifukiza mwilini.

Hicho ndicho alichowaza wakati plani ya kwanza ya kumsaka panya aliyekufa ilipofeli.

Kazi iliyobaki sasa ni kusubiri mgeni wake, ambaye angewasili muda wowote kuanzia wakati ule. Alichowaza sasa ni jinsi atakavyompokea, kuongea naye, na kila ambacho kinastahili wapenzi wanapokutana.

Pamoja na hayo alijua aibu ya ugeni kati yake na mpenzi wake itachukua nafasi. Wote watakuwa na aibu ya kukutana kwa mara ya kwanza, lakini mgeni wake itakuwa zaidi kwa sababu pia atakuwa yupo ugenini.

Ilipita robo saa toka muda wa awali walioahidiana kupita. Hakuona dalili ya mgeni yoyote. Kwa muda wote aliokuwa ndani alikuwa amevaa pensi, bila shati kwani mara nyingi anapokuwa nyumbani na hana ratiba ya kutoka hakuwa anapenda kuvaa shati wala fulana. Alichoka kukaa ndani na kuamua kutoka nje angalau dakika moja, ili arejee tena ndani.

Zilikuwa zimepotea dakika 22 hivi baada ya saa 10:00. Wakati anataka kunyanyuka, ndipo aliposikia sauti ya kugonga mlango bila sauti. Akarudi kukaa

Awali alidhani ni wale watu wa kudai pesa ya usafi ya ulinzi. Lakini ghafla akalitupia mbali wazi hilo kwa sababu watu hao ambao wanatoka kwenye ofisi za serikali za mitaa, huwa na tabia ya kuja kwa vishindo na si kwa kunyata kama hivyo.

Hodi inapigwa wakati wanakuwa wameshaingia kwenye mlango mkubwa ambaye wenyewe wanauita geti. Na wanaanza na maneno, “wenyewe mpo? Haya haya, pesa ya ulinzi na taka...”

Mara ya mwisho ugongaji huo kwenye mlango wake ulikuwa mwezi uliopita alipoagiza supu kutoka kwa mama muuza mmoja aliyekuwa jirani yao. Ni baada ya kuumwa maralia.

Baada ya kupata vipimo na kupata nafuu na kuwa na hamu ya kula alikwenda kuagiza supu ya utumbo na chapati mbili wakati haikuwa kawaida yake. Kwa sababu chapati zilikuwa bado zinachomwa, alielekeza kama ikiwa tayari aletewe nyumba ya tatu kutoka wanapouzia, pamoja na chumba anachoishi cha uani.

Mlango uligongwa na msichana mmoja aliyekuwa anafanya kazi ya kusambaza supu kwa wateja wa yule mama.

Ndivyo ulivyogongwa siku hiyo. Ulikuwa ugongaji dhaifu uliochanganyika na woga ndani yake. “Karibu.” Akaitikia. Mgongaji hakuingia. “Mlango haujafungwa na komeo, pita!” Akajibu tena. Hakuingia yeyote.

Akaamua kutaka kwenda kufungua. Wakati ananyanyuka tu, mlango ukafunguka. Aliyetaka kuingia, hakuingia moja kwa moja.

Alitanguliza kichwa kama anachungulia kwanza. Heri akatabamu. Naam! Alikuwa mgeni wake aliyekuwa akimsubiria kwa hamu, Nuru.

“Karibu Nuru.” Akamkaribisha kwa sauti yenye bashasha, lakini iliyoonekana kutoka kwa tabu mdomoni, kitu ambachi hata mwenyewe alijishangaa.

“Ahsante.” Nuru akajibu huku akiwa anaingia taratibu kwa hatua moja moja, huku akionekana hajui kama asimame, akae au afanye nini.

“Unaweza kukaa kitandani hapo? Au nikupishe kwenye kistuli?” Heri akamuuliza.

“Aaa wewe kaa tu kwenye kistuli chako. Mimi nitakaa hata hapa kitandani. Nuru aliamua kukaa kitandani kwa sababu hakukuwa na sehemu nyingine ya kukaa. Hakuwa na kochi zaidi ya kistuli tu ambacho kilikuwa kimekaliwa na mwenyewe. Hakutaka kumsumbua mwenyeji wake, akaamua tu akae kwenye kitanda ambacho kilikuwa karibu zaidi na mlango.

“Samahani nimekuweka kitandani, maana nyumba yenyewe haina hata kiti, ndiyo tunaanzaanza maisha hivyo.”

“Hakuna tabu, siku zote mwanzo mgumu mwaya.” Nuru akajibu kumpoza Heri ili kutompa unyonge.

“Hukupotea?” “Hapana, nimekuja kuuliza kumbe nimeshafika. Ile nauliza tu naambiwa nyumba hiyo hapo, ingia kwenye kigeti hicho.

Nilipoingia nikaona vyumba ya uani na wewe tayari ulishaniambia kuwa chumba chako mtu akiingia kwenye mlango mkubwa kiko upande wa kulia.”

ITAENDELEA JUMAPILI



# ALI KIBA ROHO NYEUPE

MSANII wa Bongo Fleva, Alikiba amesema kituo chake cha radio Crown FM, hakitakuwa na ubaguzi wa kupiga nyimbo za wasanii, badala yake kila mwanamuziki atajivunia kuwa nacho.

Matangazo ya Redio Crown FM yalianza kupeperuka hewani siku chache zilizopita na kusikika nyimbo za wasanii mbalimbali wakiwamo mahasimu wake na kuibua mjadala katika mitandao ya kijamii.

Akifafanua suala hilo, Alikiba amesema kuwa Crown FM haitabagua ngoma za msanii yeyote kwani ni chombo cha kila mtu akiwamo Diamond na Harmonize.

# OMONDI KUWANIA UBUNGE 2027

MCHEKESHAJI maarufu kutoka Kenya, Eric Omondi amethibitisha rasmi kuwa anajitosa katika ulingo wa siasa na atawania nafasi ya ubunge katika uchaguzi mkuu ujao mwaka 2027.

Akizungumza kupitia Kenya Online Media, Omondi amesema kwamba ataingia kwenye siasa, na atawashawishi vijana wengine kuungana naye katika kuwania nafasi mbalimbali nchini humo.

"Tutawania kwa idadi kubwa na kama hauko debeni tutakuweka kwa nguvu. Tunaenda kuanza kuzungumza kwa vijana, kuwaelimisha, kuwaunganisha pamoja na kuwaandaa kusafisha bunge la Kenya mwaka 2027," amesema Omondi

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VARANE KUACHIWA
KLABU ya Manchester United iko tayari kumwachia mlinzi wa zamani wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 31 kuondoka bure mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto. (**Mirror**)

### BARCA YAMSUBIRIA DIAZ
BARCELONA inatazamia kuimarisha safu yao ya mashambulizi huku mshambuliaji wa Liverpool na Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27, akiwa mmoja wa walengwa wao. (**Mundo Deportivo**)

### MATIP NAE KUONDOKA
MLINZI wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 32, ni mchezaji mwingine ambaye anaweza kuondoka Liverpool msimu huu wa joto huku Roma na Lazio zikimwania. (**Corriere**)

### RASHFORD HAKIELEWEKI
KLABU ya Manchester United inatarajia wachezaji kadhaa kuondoka majira ya joto ili kukidhi mahitaji ya usawa wa kifedha michezoni, huku mustakabali wa mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26, ukizingatiwa. **(Express)**

### CARLOS AVUTIWA
AC Milan inavutiwa na beki wa Aston Villa Mbrazil Diego Carlos mwenye umri wa miaka 31, baada ya kufanya vyema aliporejea kutoka kwa jeraha la mguu. (**Sport - via TeamTalk**)

### ADARABIOYO ATAKA KUONDOKA
MLINZI wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26 ameiambia klabu hiyo kuwa anakusudia kuondoka kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto, huku Liverpool, Tottenham Hotspur na Newcastle United zikivutiwa nae. (**Express)**

### MITOMA ANYATIWA
WINGA wa Brighton na Japan, Kaoru Mitoma mwenye umri wa miaka 26 ananyatiwa na klabu za Arsenal, Manchester City na Manchester United. (**Fichajes - via 90 min**)

### PSG KIZINGITI KWA YAMAL
KLABU ya Paris St-Germain inakabiliwa na kizingiti katika jaribio lao la kumsajili kinda wa Barcelona na Hispania, Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 16, huku wakala wa kinda huyo akiiambia klabu hiyo hauzwi. (**AS**)

### RIGGE AGOMBEWA
KLABU za Arsenal na Tottenham Hotspur zinatazamia kumsajili kiungo wa West Ham aliyewahi kuichezea timu ya England chini ya umri wa miaka miaka 16, Daniel Rigge. **(ESPN)**

### RANGNICK ATAJWA TENA MAN
KLABU ya Bayern Munich imethibitisha kuwa wanafanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Manchester United, Ralf Rangnick kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel kama kocha. (**Goal**)

### CONTE NA NAPOLI
KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte amefikia makubaliano ya kuchukua nafasi ya kocha wa Napoli. (**Mirror**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BEI YA OLISE YAWEKWA HADHARANI

**LONDON,** England

Anawindwa na klabu kubwa EPL, Crystal Palace yaweka msimamo...

KLABU ya Crystal Palace iko tayari kuwauza nyota wawili Eberechi Eze na Michael Olise, lakini wanataka kuanzia pauni milioni 60 kwa kila mmoja, kwa mujibu wa ripoti.

Eze na Olise wameimarisha hadhi yao ya kuwa wachezaji wawili bora zaidi wa Ligi Kuu England kwa timu za 'sita bora' katika misimu ya hivi karibuni, na inaeleweka wamehusishwa na Klabu hizo kutokana na kiwango chao.

**Wote wawili walitia saini mkataba mpya katika kipindi cha pili cha 2023 lakini hilo halijazuia wahusika kufuatiliwa maendeleo yao.**

BBC Sport imeripoti kwamba The Eagles hao watasikiliza ofa zozote zitakazotolewa kwa mchezaji yeyote msimu huu wa joto, lakini tu ikiwa zitaanza au zinazidi pauni milioni 60.

Ingawa Palace hawako tena katika hatari yoyote ya haraka ya kushushwa daraja kwenye na hawahitaji kuuza wachezaji ili kusawazisha vitabu, inakubalika kwamba Eze na Olise watakuwa chini ya maslahi ya uhamisho kutokana na hali na ubora wao.

Eze na Olise wana furaha ndani ya Palace na wana nia ya kuhakikisha kwamba kuondoka pale Selhurst Park kunalingana na masharti yao, wakitanguliza hatua ambazo zingewaruhusu kuendelea kucheza.

90min ilifichua mapema wiki hii kwamba Olise angependa kujiunga na Manchester United iwapo wataamua kuthibitisha nia yao na ofa msimu huu wa joto. Utawala uliopita wa United na ule mpya unaoongozwa na INEOS wanamshabikia Mfaransa huyo.

Hata hivyo, Chelsea haitarajiwi kufanya uhamisho mpya kwa Olise baada ya kujaribu na kushindwa kumsajili mwaka jana. The Blues walidhani walikuwa wameanzisha kipengele cha kuachiliwa huru katika mkataba wake, lakini haikuwa hivyo na walirudi nyuma kwenye makubaliano baada ya kutishiwa kuchukuliwa hatua za kisheria na Palace.

Olise aliendelea kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na kifungu cha juu zaidi lakini ngumu sawa cha kutolewa.

Eze alipendekezwa kujiunga na Manchester City msimu uliopita wa joto kabla ya kuhamia kwa Matheus Nunes wa Wolves, na pia amewavutia Arsenal, Liverpool na Tottenham Hotspur.

HABARI MICHEZO




# ARSENAL, MAN CITY ZAMTOLEA MACHO GUIMARAES

**LONDON** England

ARSENAL na Manchester City zinafahamu kwamba, Newcastle United itasikiliza ofa inayozidi pauni milioni 80 kwa Bruno Guimaraes msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Washikabunduki na City wako sokoni kutafuta kiungo wa kati kuelekea msimu wa 2024/25, na iliripoti wiki iliyopita kwamba Guimaraes ni chaguo namba moja kwao.

Ingawa kuna kipengele cha kutolewa cha pauni milioni 100 katika mkataba wa Guimaraes, 90min ilifichua kuwa kuna makubaliano ya mdomo kati ya klabu na mchezaji kusikiliza ofa za zaidi ya pauni milioni 80 kutoka kwa klabu zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

90min sasa inaelewa kuwa Arsenal na City wamejifunza kuhusu thamani hii ya chini ya Guimaraes, ingawa sio timu pekee zinazovutiwa na huduma yake. Paris Saint-Germain pia wanavutiwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

Kumekuwa na mashaka iwapo wamiliki wa PSG wa Qatar wanaweza kufanya mazungumzo na wakuu wa klabu ya Newcastle wa Saudi Arabia, lakini inaeleweka kuwa hii haiwezi kuzuia dili hilo.

Kwa mfano, PSG ilikubali ofa ya rekodi ya dunia kutoka kwa Al Hilal ya Saudia kwa Kylian Mbappe msimu uliopita wa joto, lakini fowadi huyo alikataa kuondoka Parc des Princes.

PSG walifanikiwa kumuuza Neymar kwa Al Hilal bila suala kama hilo.

Newcastle wanahitaji kuongeza pauni milioni 35 hadi 50 kupitia mauzo ya wachezaji ili kupunguza wasiwasi wa kukiuka Kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu ya England, na wangependelea kumuuza mchezaji mmoja kwa ada ya juu kuliko wachezaji kadhaa kwa fedha ndogo.

Wameweka kipaumbele kwa mshambuliaji nyota Alexander Isak, ambaye pia anavutiwa na Arsenal, ikimaanisha Guimaraes ana uwezekano mkubwa wa kuuzwa, huku mchezaji wa kimataifa wa Englan, Callum Wilson pia akiwaniwa.

# Silva bado hakieleweki Man City

**MANCHESTER,** England




MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva ana nafasi kubwa ya kuikacha klabu hiyo itakapofika mwishoni mwa msimu huu 2023/24.

Silva mwenye umri wa miaka 29, kwa muda mrefu amekuwa kitaka changamoto ya kufikiria wapi atakapocheza msimu ujao, licha ya kuwa na mkataba na Man City hadi mwaka 2026.

Taarifa zinaeleza kuwa mshambuliaji huyo ameshinikiza kuuzwa mwishoni mwa msimu huu, huku Barcelona ikitajwa kumuwania ili kuboresha kikosi chake, ambacho kinaelekea kupoteza ubingwa wa LaLiga mikononi mwa Real Madrid.

Kocha Xavi anatajwa kuwa msukumo mkubwa wa kumvuta Silva kujiunga na Barcelona, ingawa inatajwa kama tetesi kuhusu wawili hao kuwa na mazungumzo.

Hata hivyo, Barcelona huenda ikawalazimu kutoa pauni milioni 50, kama ada ya uhamisho wa Silva, ambaye alisajiliwa Man City mwaka 2017 kwa ada ya euro milioni 50.

# Zidane aonywa kuhusu Bayern

**PARIS,** Ufaransa

GWIJI wa soka wa Ufaransa, Marcel Desailly amemuonya Zinedine Zidane kuhusu mpango wa kuchukua kazi ya kukinoa kikosi cha Bayern Munich.

Zidane anatajwa kupewa kipaumbele cha kuchukua nafasi ya kuliongoza benchi la Klabu hiyo ya mjini Munich, ambaapo kwa sasa linaongozwa na Thomas Tuchel atakayeondoka mwishoni mwa msimu huu.

Desailly ameiambia Sport1 kuwa Zidane anapswa kuwa makini endapo mpango wa kupewa nafasi ya kuwa kocha mkuu Bayern Munich utafanikiwa kama inavyotajwa katika vyombo kadhaa vya habari nchini Ujerumani.

Amesema Kocha huyo ambaye alicheza naye kwenye kikosi cha Ufaransa kilichotwaa Ubingwa wa Dunia mwaka 1998, anapaswa kuwa makini katika usajili wa wachezaji na kuwaondoa baadhi ambao kwa sasa hawana msaada kwenye cha Munich.



"Bayern Munich ina wachezaji wachache wanaoweza kuzoea falsafa ya Zidane ya 4-3-3 yake. Klabu inapaswa kutumia fedha nyingi kurekebisha timu na kuibadilisha kulingana na mahitaji yake.

"Lakini kwa nini asifanye hivyo? Ikiwa Bayern kweli wanataka mabadiliko makubwa hii itakuwa fursa sahihi. Lakini hii itategemea na usajilia takaoufanya na kuwaacha baadhi ya wachezajia mbao wanaonekana hawana msaada."

## HABARI MICHEZO

# ZITAKAZOPANDA LIGI KUU, 'PLAY OFF', LIGI YA CHAMPIONSHIP KUJULIKANA LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU moja itakayoungana na Kengold kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, na mbili zitakazocheza mechi za mchujo, 'play off', zinatarajiwa kujulikana leo, wakati wa kuhitimisha kwa Ligi ya Championship, kwenye michezo nane itakapofanyika viwanja mbalimbali nchini.

Timu ya Pamba FC, ambayo ipo katika nafasi nzuri zaidi ya kupanda Ligi Kuu, itakuwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha kukipiga dhidi ya Mbuni FC.

Mabingwa hao wa Ligi ya Jamhuri ya Muungano mwaka 1990, wanahitaji ushindi tu kuweza kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kuteremka mwishoni mwa miaka ya 1990.

Pamba ambayo ina pointi 64, inahitaji ushindi ili kufikisha pointi 67, ambazo haziwezi tena kufikiwa na timu yoyote ya chini yake, hivyo kuungana na KenGold, yenye pointi 67, huku tayari ikiwa imeshakata tiketi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao, lakini leo itahitimisha mechi yake kwa kucheza na Polisi Tanzania, Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Shughuli nyingine itakuwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, wakati Mbeya Kwanza itakapoikaribisha, Transit Camp, katika mechi ambayo inaweza kuipandisha Ligi Kuu timu hiyo.

**Mbeya Kwanza ambayo inashika nafasi ya tatu kwa pointi 62, kama ikishinda mechi hiyo itafikisha 65, na kama Pamba ikifungwa na kubaki na pointi zake 64, timu hiyo itakata tiketi ya kwenda Ligi Kuu.**

Kama ikipata matokeo yoyote na Pamba ikishinda, basi moja kwa moja itapata nafasi ya kucheza 'play off' dhidi ya Biashara United ambayo ipo nafasi ya nne, ikiwa na pointi 59.

Mshindi wa mechi mbili za 'play off' nyumbani na ugenini, ataisubiri timu moja kutoka Ligi Kuu kwa ajili ya 'play off' nyingine, ambayo itaamua timu ya kupanda, kushuka au kubaki.

Biashara itacheza dhidi ya Cosmopolitan, Uwanja wa Karume, Musoma, Mara, TMA itakipiga na Copco, Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha, Pan African ipo Meja Jenerali Isamuhyo dhidi ya Stand United, Green Warriors, itacheza na Ruvu Shooting, Mabatini, Mlandizi, Pwani, na FGA itakipiga dhidi ya Mbeya City, Majimaji, Songea.



Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Joshua Nassari (kushoto) akifurahia na washindi wa mbio za Lake Manyara Marathon 2023 zilizofanyika jana wilayani humo, zikiwa na lengo la kutoa fursa mpya ya utalii ndani ya Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bondia Changalawe aingia kambini kujifua

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa mchezo wa ngumi za ridhaa, Yusuph Changalawe amesema wiki ijayo anatarajia kuanza kambi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kuwania kufuzu michuano ya Olympiki yatakayofanyika nchini Thailand kuanzia Mei 20 mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Changalawe alisema lengo lake ni kufanya vema kwenye mashindano hayo ili apate nafasi ya kwenda nchini Ufaransa kushiriki Olympiki itakayoanza Julai mwaka huu.

"Malengo yangu ni kupata nafasi ya kwenda kushiriki Olympiki nchini Ufaransa na kuweza kuipeperusha vema bendera ya Taifa," alisema Changalawe.

Bondia huyo Aliongeza kuwa mashindano hayo yanatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa kutokana na kuwa na mataifa mbalimbali.

"Mashindano yatakuwa magumu, hivyo ninapaswa kujinoa kweli kweli ili nikatimize malengo iliyojiwekea," alisema bondia huyo.

## Yanga yaanza usajili, kuacha nyota saba

INATOKA UK. 24

wa mkopo ukiwa unatamatika mwishoni mwa msimu huu, akirejea kwenye klabu yake mama.

Hata hivyo, imeelezwa kuwa beki huyo wa kulia anawaniwa na klabu ya Simba ambaye imeshapiga hodi Singida Fountaine Gate, ambayo inadai kuwa mchezaji huyo ana thamani ya Sh milioni 200.

## Benchikha adaiwa kuomba kuondoka

INATOKA UK. 24

wetu, uongozi umeridhia maombi yake licha ya Mwekezaji, Mohammed Dewji (Mo) kutaka kuendelea na Benchikha kwa msimu mwingine.

"Suala la Benchikha kubaki kwa msimu ujao limekuwa gumu licha ya maombi ya mwekezaji na tayari mchakato wa kupata kocha mpya umeanza mapema," alisema mtoa habari wetu.

Aliongeza: "Msimu wa 2024/25 anakuja kocha mwingine, Benchikha anaondoka na inadaiwa kwamba anawaniwa na timu ya taifa ya Algeria," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa mchakato kumpa mrithi wa Benchikha utaanza mapema ili atakapoondoka kocha huyo wawe tayari na mtu wa kumtambulisha.

Alipoulizwa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally kuhusuiana na suala la Benchikha, alisema, "Sifahamu suala lolote kuhusu suala la kuondoka kwa Benchikha, ninachojua kwamba yeye ni kocha wetu, kikubwa tunapambana kuhakikisha tunashinda mechi zetu zote zilizobaki," alisema Ahmed.

Wakati huo huo, mtoa habari huyo alisema kwa sasa mchezaji yeyote wakitaka kumsajili lazima wajumbe ambao wako kwenye kamati ya kumshauri Dewji (hawakupenda kuyataja majina yake) waende nae kwake kwa ajili ya kusaini mkataba.

Alieleza kuwa wameanza kufanya kazi kimya kimya likiwemo suala la kocha mpya pamoja na kuwa kwenye program mpya kwa ajili ya kusaka wachezaji kwa ajili ya usajili kwa msimu ujao.



# Michezo

Jumapili Aprili 28, 2024
Nipashe




Bei ya Olise yawekwa hadharani UK. 21




Mchezaji wa Mamelodi Sundowns, Khuliso Mudau (kushoto) akiwania mpira dhidi ya Rodriguez Silva wa ES Tunis wakati wa mchezo wa pili wa nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Afrika baina ya timu hizo, kwenye uwanja wa Loftus Versfeld mjini Pretoria nchini Afrika Kusini juzi Ijumaa. Mamelodi walifungwa 2-0 na hivyo kuifanya ES Tunis kutinga fainali na itacheza na Al Ahly ambayo iliifunga TP Mazembe mabao 3-0 kwenye nusu fainali nyingine. **PICHA: MITANDAO**

# YANGA YAANZA USAJILI, KUACHA NYOTA SABA

**Na Adam Fungamwango**

## Yatamba imeshaanza mkakati wa kukabiliana na chochote kitakacho...

WAKATI ikiwa kwenye nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, Klabu ya Yanga imeanza mchakato wa usajili kimya kimya kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, huku ikitarajia kuacha wachezaji saba.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa ipo kwenye mazungumzo na wachezaji kadhaa kutoka pande mbalimbali za Afrika, lakini mazungumzo yanakwenda vizuri kwa wachezaji watano ambao kama mambo yatakwenda vizuri wanaweza kuvaa jezi ya njano na kijani msimu ujao.**

Kwa mujibu wa mtoa taarifa huyo, wachezaji hao ni winga hatari wa Petro de Luanda ya Angola, Deivi Miguel Vieira maarufu kama, Gilbetro, Cheick Diakite wa Real Bamako ya Mali, ambaye wakati mwingine hucheza kama straika na winga ya kushoto.

Wengine ni winga wa kulia wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Phillippe Kinzumbi, Abubeker Nassir Ahmed raia wa Ethiopia, anayeichezea Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini nafasi ya straika, na Ranga Chivaviro, straika wa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, ambaye klabu hiyo ilimkosa dakika za mwisho msimu uliopita.

"Tunajua kuwa tutaacha baadhi ya wachezaji, maisha ya soka yanajulikana, tunaweza kuondokewa na baadhi ya wachezaji tegemeo, lakini kwa sababu uongozi ni imara, tayari umeshaanza mkakati wa kukabiliana na chochote kitakachotokea, ikitokea mchezaji akiondoka, tutatafuta mbadala wake ambaye uwezo wake ni kama aliyeondoka au zaidi, hatusubiri hadi timu ifanye vibaya ndiyo tuanze kuona mapungufu, Yanga imeshapita huko," alisema mtoa taarifa huyo.

Mmoja wa wachezaji ambao inasemekana huenda akaondoka ni kinara wa mabao katika timu hiyo na Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ujumla, Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki, ambaye anatakiwa na klabu mbalimbali kubwa barani Afrika, huku Mamelodi Soundowns, ndiyo inayoonekana kumtolea macho zaidi.

Pia, Yanga inatarajiwa kuacha baadhi ya wachezaji ambao watawapisha wenzao wapya watakaosajiliwa.

Chanzo kimesema kuwa, wachezaji saba ambao wanatarajia kuondoka mwishoni mwa msimu ni Mahlatsi Makudubela 'Skudu', Gift Fred, Zawadi Mauya, Bakari Mwamnyeto, Keneddy Musonda, Augutine Okra ambaye alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili na Nickson Kibabage ambaye yupo kwa mkopo akitokea Singida Fountain Gate, huku muda wake

INAENDELEA UK 23

## Benchikha adaiwa kuomba kuondoka Simba

**Na Saada Akida**

IMEELEZWA kuwa Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha huenda msimu ujao asiwepo kwenye benchi la ufundi la Wekundu hao wa Msimbazi baada ya kupata ofa ya kuinoa timu ya Taifa ya Algeria.

Taarifa za ndani ambazo bado hazijathibitishwa mapema jana zilisema kwamba, Benchikha tayari amewasilisha barua ya kuomba kuondoka katika Klabu hiyo.

Kwa mujibu wa tarifa hizo, Benchikha ameutaka uongozi kutoendelea kukinoa kikosi cha Simba kwa msimu ujao na kwa ajili ya kwenda kutafuta changamoto nyingine likiwemo dili hilo ambalo lipo mezani.

Kwa mujibu wa mtoa habari

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042